SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR**

# SERA YA UVUVI YA ZANZIBAR 2022



# SERA YA UVUVI YA ZANZIBAR 2022

2022

Sera ya Uvuvi ya Zanzibar 2022 iliandikwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar. Ilichapishwa kwa msaada wa Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini Tanzania.

Picha kwa hisani ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar

# DIBAJI

Sekta ya Uvuvi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Zanzibar pamoja na maendeleo ya Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Sekta hii inaweza kuchangia zaidi katika uchumi wa taifa endapo usimamizi na udhibiti utaimarishwa na kutekelezwa kwa ufanisi na uadilifu zaidi. Kwa muktadha huu, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU) imeandaa Sera ya Uvuvi ya Zanzibar ambayo ndio chombo kikuu cha kutekeleza matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali za baharini kusudi kuchochea mabadiliko jumuishi katika maendeleo ya uvuvi.

Uvuvi ni sekta muhimu katika uchumi wa Zanzibar ikichangia asilimia 5.1 ya Pato la Taifa (GDP). Samaki ndio chanzo kikuu cha madini ya protini inayotokana na wanyama kwa wakaazi wengi wa Zanzibar. Kwa wastani kila mtu hutumia takribani kilo 23 za samaki kwa mwaka, kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na wastani wa Bara la Afrika wa kilo 9.4 kwa kila mtu kwa mwaka. Aidha, sekta ya uvuvi ina jukumu kubwa la kuinua kiwango cha uzalishaji wenye tija ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuimarisha soko la nje ya nchi kwa kusafirisha bidhaa za baharini. Sera hii inaelekeza katika kuzikabili changamoto za uzalishaji pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia ufugaji wa samaki na kilimo cha mazao ya baharini, usindikaji, uongezaji thamani na masuala ya masoko kwa jamii za ukanda wa pwani.

Lengo kuu la Sera ya Uvuvi ya Zanzibar ni kukuza maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi, kusudi iweze kuchangia kwenye maendeleo ya Uchumi wa Buluu, uhakika wa chakula, ustawi wa jamii, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za baharini pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Sera hii inalenga kuimarisha mfumo wa udhibiti na usimamizi wa sekta ya uvuvi ili kuibadilisha kutoka uvuvi wa kujikimu kuwa shughuli ya kibiashara na yenye ushindani.

.

Mhe. Suleiman Masoud Makame
WAZIRI,
WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

# SHUKURANI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU) inatambua na kuthamini juhudi kubwa za wadau wote kwa mashirikiano na michango yao adhimu katika utayarishaji wa Sera ya Uvuvi ya mwaka 2022. Wizara pia inatoa shukurani za dhati na za kipekee kwa Benki ya Dunia kupitia Programu ya SWIOFish kwa ufadhili katika matayarisho ya Sera hii.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inapenda pia kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundi, Asasi za Kiraia na jumuia za wavuvi kwa kushiriki kikamilifu kwenye matayarisho ya Sera hii. Ni imani yetu kwamba Sera hii itaongoza na kuelekeza matumizi na usimamizi endelevu wa rasilimali za baharini na ukanda wa pwani kwa ustawi wa Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, WUBU inatoa wito kwa wadau wote wa sekta ya uvuvi kuchukua hatua stahiki katika kufahamu majukumu na dhamana zao na kuitekeleza Sera hii ipasavyo.

Mwisho, tunatoa shukurani za dhati kwa kikosi cha wataalamu wa WUBU kwa juhudi kubwa walizochukuwa katika kutayarisha sera hii.

Dkt. Aboud Suleiman Jumbe

KATIBU MKUU,
WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

# YALIYOMO


**DIBAJI** . . . . . . . . **V**

**SHUKURANI** . . . . . . . . **VII**

**UFUPISHO WA YALIYOMO** . . . . . . . . **XI**

**TAFSIRI YA MANENO** . . . . . . . . **XIII**

## SURA YA KWANZA UTANGULIZI 1

1.1 USULI . . . . . . . . 1

1.2 UPEO WA SERA . . . . . . . . 1

1.3 MAWANDA YA SERA . . . . . . . . 2

1.4 MAFUNGAMANO YA SERA NA MIONGOZO MINGINE YA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA . . . . . . . . 2

1.5 1.4.2 MAFUNGAMANO YA KITAIFA . . . . . . . . 3

## SURA YA PILI HALI HALISI 7

2.1 UTANGULIZI . . . . . . . . 7

2.2 USIMAMIZI WA UVUVI . . . . . . . . 7

2.3 MAENDELEO YA KILIMO CHA MAZAO YA BAHARINI . . . . . . . . 9

2.4 ULINZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA BAHARINI . . . . . . . . 10

2.5 UTAFITI NA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA BAHARINI . . . . . . . . 11

2.6 UPATIKANAJI WA SOKO, ONGEZEKO LA THAMANI NA MIUNDOMBINU . . . . . . . . 12

2.7 HOJA MTAMBUKA . . . . . . . . 14

## SURA YA TATU DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA 15

3.1 UTANGULIZI . . . . . . . . 15

3.2 DIRA NA DHAMIRA YA SERA . . . . . . . . 15

3.3 MALENGO YA SERA . . . . . . . . 15

3.4 MISINGI ELEKEZI . . . . . . . . 16

## SURA YA NNE HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA 17

4.1 UTANGULIZI . . . . . . . . 17

4.2 USIMAMIZI WA UVUVI . . . . . . . . 17

4.3 MAENDELEO YA KILIMO CHA MAZAO YA BAHARINI . . . . . . . . 19

4.4 ULINZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA BAHARI . . . . . . . . 20

4.5 TAFITI KWA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA BAHARI . . . . . . . . 21

4.6 UPATIKANAJI WA MASOKO, ONGEZEKO LA THAMANI, MIUNDOMBINU, UDHIBITI WA UBORA NA VIWANGO . . . 23

4.7 HOJA MTAMBUKA . . . . . . . . 24

## SURA YA TANO MFUMO WA KISHERIA NA KITAASISI WA SERA 27

5.1 MFUMO WA KITAASISI . . . . . . . . 27

5.2 MFUMO WA KISHERIA . . . . . . . . 27

5.3 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WASHIRIKI WAKUU WA SERA . . . . . 27

## SURA YA SITA UFUATILIAJI NA TATHMINI 31

6.1 MFUMO WA UTEKELEZAJI . . . . . 31
6.2 UFUATILIAJI NA TATHMINI . . . . . 31
6.3 MAPITIO YA SERA . . . . . 31
6.4 GHARAMA NA RASILIMALI FEDHA . . . . . 31
6.5 MKAKATI WA MAWASILIANO . . . . . 31
6.6 RASILIMALI WATU . . . . . 31

# UFUPISHO WA YALIYOMO

| | |
|---|---|
| AIMS | Mkakati Jumuishi wa Usafiri wa Baharini wa Umoja wa Afrika |
| AU | Umoja wa Afrika |
| CBOs | Taasisi za Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CEDAW | Azimio la Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto |
| CHABAMCA | Hifadhi ya Bahari eneo la Changuu-Bawe |
| CITES | Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya Viumbe na Mimea Bahari Waliohatarini Kutoweka |
| CMORDBS | Kituo cha Utafiti na Kanzidata ya Hifadhi ya Bahari |
| DRC | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo |
| DSFA | Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu |
| EAMFRO | Shirika la Utafiti wa Uvuvi wa Baharini la Afrika Mashariki |
| EEZ | Ukanda Maalumu wa Uchumi |
| FAD | Matumbawe Bandia |
| FAO | Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa |
| GDP | Pato la Taifa |
| ICZM | Usimamizi Endelevu wa Maliasili za Ufukweni na Baharini |
| IMO | Shirika la Kimataifa la Baharini |
| IMS | Taasisi ya Sayansi za Bahari |
| IORA | Jumuiya ya Nchi Zilizopo Kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi |
| KMKM | Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo |
| LGAs | Serikali za Mitaa |
| MBCA | Hifadhi ya Ghuba ya Menai |
| MCAs | Maeneo ya Hifadhi ya Bahari |
| MCS | Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi |
| MIMCA | Hifadhi ya Bahari eneo la Mnemba |
| MSP | Upangaji wa Matumizi wa Maeneo ya Bahari |
| MSY | Kiwango cha Juu cha Mavuno |
| MTEF | Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi |
| NGOs | Asasi Zisizo za Kiserikali |
| OCGS | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |
| PECCA | Hifadhi ya Bahari ya Mkondo wa Pemba |
| PFRS | Sera na Mkakati wa Afrika wa Mageuzi ya Uvuvi na Kilimo cha Mazao ya Baharini |
| PPP | Mashirikiano ya Taasisi za Umma na Binafsi |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |

| | |
|---|---|
| SDGs | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SFCs | Kamati za Uvuvi za Shehia |
| SIDS | Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo |
| SME | Biashara Ndogo na za Kati |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SWIO | Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi |
| SWIOFish | Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi |
| TASAC | Shirika la Uwakala wa Meli - Tanzania |
| TUMCA | Hifadhi ya Bahari ya Tumbatu |
| TZS | Shilingi za Kitanzania |
| UKIMWI/VVU | Upungufu wa Kinga ya Mwili/Virusi Vya Ukimwi |
| UNCLOS | Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Sheria za Bahari |
| WUBU | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi |
| ZADEP | Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar |
| ZAFIRI | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar |
| ZMA | Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar |
| ZRA | Ajenda ya Utafiti Zanzibar |

# TAFSIRI YA MANENO

**Ufugaji na mazao ya baharini** – Ufugaji, ukulima au juhudi za kuzalisha samaki, viumbe na mimea katika mazingira ya bahari

**Matumbawe** – Mkusanyiko wa asili wa mawe laini yasiyo kuwa na uhai na hupatikana katika maji madogo

**Miamba** – Mawe magumu yanayopatikana baharini kwa njia ya asili au isiyo ya asili

**Viumbe adimu** – Mimea au wanyama bahari ikihusishwa pia mawe, miamba, matumbawe, na makombe ambayo vipo hatarini kutoweka kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya Viumbe na Mimea Bahari Waliohatarini Kutoweka (CITES)

**Uvuvi** – Uvunaji wa samaki katika maji chumvi au maji baridi ikiwa ni pamoja na uvunaji wa mazao ya baharini

**Uvuvi wa viwanda** – Shughuli za uvuvi zinazohusisha usarifu wa maliasili za baharini

**Maji ya ndani** – Eneo la bahari kuanzia ufukwe wa maji ya kitaifa na mpaka baina ya Zanzibar na Tanzania Bara;

**Rasiliamali za bahari** – Rasilimali ambazo hupatikana ndani ya bahari, kama vile bioanuai, mafuta, mchanga na matumbawe;

**Kusarifu samaki** – kusafishwa, kukaushwa, kuanikwa, kuhifadhiwa kwenye barafu, makopo, mikebe, kutiwa chumvi au njia nyenginezo za kusarifu samaki ili kufikishwa sokoni;

**Maji ya kitaifa** – Eneo la bahari kuanzia masafa ya meli 12 kutoka maji ya ndani au mwambao wa visiwa vya Zanzibar.





# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 USULI

Sera ya Uvuvi imeandaliwa kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ambayo inaelekeza kuibadilisha sekta ya uvuvi kutoka uvuvi wa kujikimu na kuwa wa kibiashara na wenye ushindani. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mkazo katika kuweka mazingira bora ya utawala na uratibu wa sera na sheria ili kuchochea mabadiliko jumuishi katika maendeleo ya uchumi wa viwanda, sayansi na teknolojia. Sera inalenga kuitafsiri kwa vitendo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 kwa kuongeza thamani yabidhaa za viwandani, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini wenye tija na kuimarisha huduma za soko la ndani na nje. Sera inasimamia maendeleo ya uvuvi, uhifadhi wa bahari, na utafiti wa rasilimali za baharini.

Sera inatoa mwongozo kwa watendaji wote kwenye sekta ya uvuvi kuimarisha mnyororo wa thamani kwa kuinua viwango vya uzalishaji wenye tija, kuongeza thamani kupitia usarifu wa bidhaa za uvuvi, kuimarisha huduma za masoko, kuinua kipato na kuboresha uhakika wa chakula na lishe, kuongeza ajira na fedha za kigeni pamoja na usimamizi endelevu wa raslimali za uvuvi ili kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuwekeza kwenye sekta ya uvuvi. Uwekezaji huu utaongeza upatikanaji wa huduma bora na kukuza matumizi ya teknolojia za uvuvi, ongezeko la thamani, huduma za kifedha na kuunganisha masoko kupitia ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu.

*Uvuvi unaajiri watu zaidi ya 78000, sawa na 8.5% ya nguvukazi ya Zanzibar.*

Sekta ya Uvuvi ya Zanzibar inajumuisha uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini ambapo kwa sehemu kubwa ni uvuvi mdogo mdogo na ukulima wa mwani. Jumla ya samaki waliovuliwa mwaka 2021 ni tani 47,114.6, wakiwa na thamani ya TZS milioni 237,148. Pamoja na kupungua kwa mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa kutoka asilimia 6.6 mwaka 2012 mpaka asilimia 5.1 mwaka 2021 (OCGS, 2021), sekta hiyo ni muhimu kwa uhakika wa chakula na upatikanaji wa ajira na kupunguza umasikini. Mzunguko mzima wa mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi unaajiri kiasi ya watu 78,859 ambao ni sawa na asilimia 8.5 ya nguvu kazi ya Zanzibar (OCGS, 2021).

## 1.2 UPEO WA SERA

Mwaka 2002, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitayarisha Sera ya Kilimo ambayo ilijumuisha sekta ndogo za kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na ushirika na mazingira. Kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia, mifumo ya uzalishaji, mabadiliko ya hali ya hewa na kasi ya maendeleo katika sekta ya kilimo, Sera mpya zimeundwa ambazo awali zilikuwa sehemu ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2002. Sera hizo ni pamoja na Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar (2008), Sera na Programu ya Maendeleo ya Mifugo (2012), Sera ya Masoko ya Kilimo (2012) na Mkakati wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Kilimo cha Samaki na Mazao ya Baharini (2016).

*Mwaka 2022, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliandaa Sera ya Uchumi wa Buluu ili kutekeleza Dira ya Zanzibar ya 2050*

Mwaka 2022, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitayarisha Sera ya Uchumi wa Buluu ili kufikia malengo ya Dira ya Zanzibar ya 2050. Sera hiyo inasisitiza uwekezaji endelevu kwenye sekta ya uvuvi. Utekelezaji wa dhana ya Uchumi wa Buluu utaimarisha maendeleo ya uchumi, na kuhakikisha kuwa kupitia mnyororo wa thamani, sekta ya uvuvi inayoajiri asilimia 8.5 ya nguvukazi ya Zanzibar. Shughuli za uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini zimeorodheshwa kati ya vipaumbele vitano vya utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar. Kuundwa kwa Sera ya Uvuvi Zanzibar unaenda sambamba na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, kikanda na kitaifa kwa lengo la kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

## 1.3 MAWANDA YA SERA

Sera ya Uvuvi inaelekeza kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi, pamoja utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika eneo la bahari ya Zanzibar. Kadhalika, Sera inalenga katika kuwawezesha wavuvi kuvua katika maji ya kina kirefu na bahari kuu. Pia Sera inakusudia kuweka mazingira mazuri yatakayoiwezesha sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za uzalishaji, usarifu, uongezaji wa thamani na huduma za masoko. Sera pia imeweka mkazo kwenye umuhimu wa uhifadhi wa Bahari, ushikirishwaji wa wadau, matumizi ya technolojia ya habari na masoko. Aidha, Sera imezingatia umuhimu wa tafiti wa bahari pamoja na maendeleo ya miundombinu ya sekta ya uvuvi. Ili kufikia malengo hayo, Sera imesisitiza kuzingatia masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, kujenga uwezo wa kitaasisi, ushirikishwaji wa taasisi binafsi na za umma katika utoaji wa huduma.

## 1.4 MAFUNGAMANO YA SERA NA MIONGOZO MINGINE YA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA

Sera ya Uvuvi ya Zanzibar imeandaliwa kwa kuzingatia mafungamano ya mifumo ya miundo ya usimamizi wa rasilmali za pwani kitaifa, kikanda na kimataifa. Sera, miongozo, mikataba na mikakati mbali mbali katika kusimamia na kuendeleza mazingira ya pwani na rasilimali zake ni pamoja na:

### 1.4.1 MAFUNGAMANO YA KIMATAIFA NA KIKANDA

#### 1.4.1.1 Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Sheria za Bahari (UNCLOS)

Mkataba huu unahusisha masuala ya kisheria ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani. Mkataba huo unahusisha usafirishaji wa baharini na majukumu ya mataifa wanachama, pamoja na maeneo ya bahari na rasilimali zake.

#### 1.4.1.2 Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)

Lengo la 14 linaelekeza uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake, na linaunganishwa na Lengo la 1 (Kutokomeza Umasikini wa Aina Zote Kila Mahali); Lengo la 2 (Kutokomeza Njaa, Kuwa na Uhakika wa Chakula, Lishe Bora na Kukuza Kilimo Endelevu); Lengo la 5 (Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana Wote); Lengo la 7 (Nishati Mbadala kwa Gharama Nafuu); Lengo la 8 (Mazingira Bora ya Kazi na Kukuza Uchumi) and Lengo la 13 (Amani, Utu na Usawa kwenye Sayari yenye Afya).

#### 1.4.1.3 Malengo ya Agenda ya Umoja wa Afrika (AU) ya 2063

Kupitia Tarajio la Kwanza la Agenda ya Umoja wa Afrika ya 2063, Sekta ya Uvuvi imefungamana na Lengo la 6 ambalo linaelekeza kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa bahari kupitia uvuvi wa kisasa utakaoinua kiwango cha uzalishaji, tija, na ongezeko la thamani. Kadhalika, Lengo la 7 linaelekeza utunzaji wa mazingira kwa ajili ya uwepo wa hali ya hewa endelevu na uchumi himilivu wa jamii.

#### 1.4.1.4 Mkakati Jumuishi wa Usafiri wa Baharini wa Umoja wa Afrika (AIMS) wa 2050

Lengo kuu la Mkakati ni kuimarisha ukuaji wa uchumi wa baharini na maeneo ya pwani ya Afrika kupitia uwekezaji endelevu na utekelezaji wa mikakati jumuishi ya uchumi wa buluu inayozingatia matumizi sahihi ya rasilimali na uhifadhi wa mazingira ya pwani.

#### 1.4.1.5 Mkakati wa Uchumi wa Buluu wa Umoja wa Afrika

Mkakati unaelekeza kwenye matumizi jumuishi ya elimu, ujuzi na teknolojia katika shughuli za uvuvi, ufugaji wa samaki na mazao ya baharini, utalii, nishati, usafiri wa baharini, madini, na utafiti katika kufanikisha uvuvi endelevu, uhifadhi wa mazingira, kukabiliana na hali ya hewa, na ushirikishwaji wa jamii

#### 1.4.1.6 Itifaki ya Uvuvi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)

Itifaki inalenga kwenye uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali hai za majini na mifumo ya ikolojia ya majini kwa maslahi ya nchi wanachama wa Jumuia walioridhia Itifaki hii.

#### 1.4.1.7 Mkataba wa Lomé

Mkataba unashughulikia utulivu na usalama wa baharini na kukuza matumizi endelevu ya rasilimali kwa kuzuia na kupambana/kutokomeza uvuvi haramu usioripotiwa na usiodhibitiwa (IUU), uchafuzi wa mazingira ya baharini, uhalifu wa baharini pamoja na kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema, kuuratibu, kutoa mafunzo,

kujenga uwezo, pamoja na utunzaji endelevu wa bioanuwai ya baharini na pwani.

#### 1.4.1.8 Maazimio ya Jumuiya ya Nchi Zilizopo Kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) Katika Kutekeleza Dhana ya Uchumi wa Buluu

Jumuiya inaratibu na kuimarisha uvunaji endelevu wa rasilimali za bahari, uwezeshaji wananchi kiuchumi, uhifadhi wa mazingira ya bahari, kuhifadhi rasilimali zilizopo kwenye bahari hususan kwenye ukanda wa bahari kuu, pamoja na kufanikisha utekelezaji wa masuala ya uchumi wa buluu miongoni mwa nchi wanachama.

#### 1.4.1.9 Sera na Mkakati wa Afrika wa Mageuzi ya Uvuvi na Kiliimo cha Mazao ya Baharini (PFRS)

Sera na Mkakati wa Mageuzi unazingatia utekelezaji wa shughuli za uvuvi na kunufaika kwa fursa zinazohusiana na uimarishaji/uboreshaji wa maisha, na kwa kutambua kwamba uvuvi endelevu unategemea utawala bora wa baharini.

#### 1.4.1.10 Azimio la Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (CEDAW)

Azimio linazitaka nchi wanachama kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na kukuza haki kwa lengo la kuleta usawa wa kijinsia.

## 1.5 1.4.2 MAFUNGAMANO YA KITAIFA

#### 1.5.1.1 Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050

Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 inalenga kuboresha maslahi ya jamii na kuinua hali ya maisha kiuchumi kufikia viwango vya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2050, pamoja na kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za pwani na baharini kwa ajili ya faida ya kizazi cha sasa na vijavyo. Dira ya 2050 inaiunganisha sekta ya uvuvi kwa kutoa ufafanuzi na mwongozo wa matumizi endelevu na mgawanyo wa rasilimali kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

#### 1.5.1.2 Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026

Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2021-2026 umedhamiria kuviwezesha visiwa vya Zanzibar kuzitumia fursa zake kufanya mageuzi ya kijamii na kiuchumi kupitia wito wa "Kuimarisha Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi"

#### 1.5.1.3 Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020 – 2025)

Sura ya 162(f) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 inazungumzia utekelezaji wa Uchumi wa Buluu kwa matumizi endelevu katika sekta za uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini, usafiri na huduma za baharini, miundombinu, ulinzi na usalama wa maeneo ya bahari, mpango mkuu wa matumizi ya bahari, utafutaji wa mafuta na gesi asilia,vyanzo mbadala vya nishati ya baharini, na utalii.

#### 1.5.1.4 Sera ya Uchumi wa Buluu ya Zanzibar (2022).

Sera ya Uchumi wa Buluu imeweka maeneo matano ya kimkakati, ikiwemo shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini, na inalenga kuinua uchumi jumuishi, ustawi wa jamii, na usimamizi endelevu wa mazingira ya pwani. Sera pia inaelekeza mikakati ya kuzikabili changamoto kupitia mbinu kamilifu na endelevu zinazofaa kimazingira za maendeleo ya matumizi makubwa ya kiuchumi ya rasilimali za pwani kwa maslahi ya Taifa.

Sera ya Uvuvi ya Zanzibar ina uwiano mkubwa na Sera ya Uchumi wa Buluu katika kuimarisha shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini kwa kutumia rasilimali za bahari na fukwe kwa njia endelevu za kulinda na kuhifadhi ikolojia ya bahari na mwambao, pamoja na upatikanaji wa takwimu na taarifa za uhakika zitakazotumika kwenye kufanya maamuzi juu ya matumizi, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na mazao ya baharini.

Sambamba na maelekezo ya Sera ya Uchumi wa Buluu, Sera ya Uvuvi itaendeleza usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazao ya baharini, utafiti na maendeleo ya teknolojia, pamoja na upatikanaji wa mitaji na masoko ya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini.

#### 1.5.1.5 Sera ya Misitu ya Zanzibar (1995)

Sera inatilia mkazo uhifadhi wa bioanuwai, utunzaji wa ardhi na ulinzi wa vyanzo vya maji, kusimamia na kulinda mfumo na ikolojia ya mikoko, pamoja na ulinzi wa viumbe na mimea bahari.

#### 1.5.1.6 Sera ya Sekta ya Kilimo (2002)

Sera ya Kilimo inasisitiza uwezeshwaji wa jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kilimo, na hivyo ni muhimu kwa maendeleo ya uvuvi endelevu.

#### 1.5.1.7 Sera ya Maji ya Zanzibar (2004)

Sera inalenga kuimarisha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama na kuhakikisha ulinzi wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na maeneo ya chepechepe yenye miamba ya matumbawe na yenye maji chini ya ardhi.

#### 1.5.1.8 Sera ya UKIMWI/VVU ya Zanzibar (2004)

Sera inalenga kukinga na kuepusha maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na upatikanaji wa huduma husika kwa waathirika kwenye jamii za wavuvi.

#### 1.5.1.9 Sera ya Habari ya Zanzibar (2005)

Sera inaimarisha uelewa wa jamii na taaluma, ikiwemo upatikanaji wa taarifa za shughuli za maendeleo ya uvuvi.

#### 1.5.1.10 Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Zanzibar (2005)

Sera inalenga kukuza uelewa pamoja na kujenga uwezo wa ujasiriamali miongoni mwa vijana. Manufaa ya utaratibu huu ni pamoja na kutolewa mafunzo ya ubunifu,ujasiriamali, upatikanaji wa mitaji, vifaa pamoja na huduma za masoko katika sekta za uvuvi.

#### 1.5.1.11 Sera ya Biashara (2006)

Sera inasisitiza mfumo wa ushirikishwaji wa jamii katika kuimarisha uwekezaji, kuongezeka kwa wawekezaji wa ndani, na matumizi endelevu ya teknolojia katika kuendesha biashara.

#### 1.5.1.12 Sera ya Uwekezaji (2005)

Sera inashajiisha uwekezaji katika viwanda vya kusarifu bidhaa za mazao ya baharini na kutoa fursa za uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu. Sera pia imetilia mkazo haja ya kurahisisha upatikanaji wa vibali na leseni za uwekezaji kupitia mfumo wa "kituo kimoja cha huduma" chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji, Zanzibar (ZIPA).

#### 1.5.1.13 Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006)

Sera ina umuhimu mkubwa kwenye kuunganisha shughuli za uvuvi na utawala shirikishi, na katika kuratibu mafunzo ya utawala, uhifadhi, usimamizi na matumizi sahihi ya rasilimali na mazingira ya pwani.

#### 1.5.1.14 Sera ya Ajira (2008)

Sera inaelekeza ukuzaji wa fursa za ajira katika shughuli za uvuvi ili kuondoa umasikini kwa wanajamii. Sera pia inatambua mchango mkubwa wa sekta ya uvuvi kama chanzo muhimu cha ajira kwa jamii, hasa kwa wanawake na vijana. Sera inasisitiza uwekezaji zaidi wa sekta binafsi ili kustawisha uchumi wa Taifa na kuongeza fursa za ajira.

#### 1.5.1.15 Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar (2008)

Sera inaimarisha ustawi na uhakika wa kupata chakula cha kutosha, salama na chenye virutubisho pamoja na kuthibitisha ubora wa chakula. Sera pia inatambua kuwa jitihada za kuimarisha uhakika wa chakula na lishe zitachangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la samaki na bidhaa za mazao ya baharini kutokana na uwekezaji endelevu kwenye sekta ya uvuvi.

#### 1.5.1.16 Sera ya Usafirishaji (2008)

Sera inaunga mkono jitihada za uwekezaji wa miundombinu ya baharini inayohusiana na shughuli za uvuvi, kama vile ujenzi wa madiko, chelezo, pamoja na utoaji wa huduma za biashara, ulinzi na usalama.

#### 1.5.1.17 Sera ya Nishati ya Zanzibar (2009)

Sera inasisitiza mifumo ya nishati salama, endelevu na ya bei nafuu. Sera pia inalenga kukidhi mahitaji ya nishati kwa sekta za ukuzaji wa uchumi, ikiwemo sekta ya uvuvi.

#### 1.5.1.18 Sera ya Utawala Bora ya Zanzibar (2011)

Sera inaelekeza kuoanisha jukumu la uhifadhi na usimamizi wa shughuli za uvuvi na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

#### 1.5.1.19 Sera ya Kukabiliana na Maafa (2011)

Sera inaelekeza kwenye kukabili majanga kutokana na mafuriko, tufani, ukame, moto, ajali za baharini, ucha-

fuzi wa mazingira ya baharini na maeneo ya pwani, ukataji wa mikoko, taka na, viatilifu vyenye sumu.

### 1.5.1.20 Sera ya Afya ya Zanzibar (2011)

Sera inasimamia uhakiki na uthithibitishwaji wa ubora wa viwango kwa bidhaa zote za majini zinazoingizwa nchini na zinazo safirishwa nje ya nchi

### 1.5.1.21 Sera ya Serikali za Mitaa ya Zanzibar (2012)

Sera inaziwezesha serikali za mitaa kuratibu na kutekeleza majukumu yao katika kufanikisha mipango ya maendeleo ya Kitaifa.

### 1.5.1.22 Sera ya Mazingira ya Zanzibar (2013)

Sera, kwa kushirikiana na vyombo vyengine, inalenga kulinda na kusimamia uhifadhi wa mazingira wa baharini na maeneo ya pwani, kuzuia na kudhibiti umwagaji wa taka na kemikali zenye sumu, kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji, pamoja na kupunguza athari mbaya za kimazingira zinazoweza kujitokeza.

### 1.5.1.23 Sera ya Masoko ya Kilimo ya Zanzibar (2013)

Sera inashajiisha upatikanaji wa rasilimali na nyenzo mbalimbali katika kukuza huduma za masoko yanayohusika na shughuli za sekta ya uvuvi.

### 1.5.1.24 Sera ya Teknolojia ya Habari na Maelezo ya Zanzibar (2013)

Teknolojia ya habari na mawasiliano ina nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko ya teknolojia na masuala mbali mbali ya utandawazi, pamoja na kuimarisha kanzi data mbali mbali kwa ajili ya kurahisisha suala zima la kufanya maamuzi kwa wakati mwafaka. Kwa mantiki hii, teknolojia ya habari ina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya uvuvi.

### 1.5.1.25 Sera ya Mashirikiano ya Taasisi za Umma na Binafsi (PPP) ya Zanzibar (2014)

Sera inaimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi katika uwekezaji, masuala ya fedha, ujenzi wa miundombinu ya kisasa, na utoaji wa huduma.

### 1.5.1.26 Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Zanzibar (2014)

Sera inaimarisha uwezeshaji wa jamii katika kufanya maamuzi shirikishi, ushirikishwaji wa masuala ya kijinsia, na maendeleo ya vyama vya ushirika.

### 1.5.1.27 Mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2014)

Mkakati umetoa miongozo katika kuongeza uwezo wa kukabili mabadiliko ya tabianchi na majanga mbalimbali ya baharini na maeneo ya pwani, kama mafuriko, kuongezeka kwa kima cha maji ya bahari, kuingia maji ya chumvi katika mashamba ya wananchi, ongezeko la joto, ukame, wadudu waharibifu,maradhi, pamoja na ndege waharibifu.

### 1.5.1.28 Sera ya Mafuta na Gesi ya Zanzibar (2016)

Sera inajumuisha mikakati na miongozo ya uvumbuzi na matumizi endelevu ya rasilimali za mafuta na gesi. Uvumbuzi wa mafuta na gesi baharini unahusiana na shughuli nyengine za uchumi wa buluu kama vile Mpango Mkuu wa Matumizi ya Bahari, uvuvi na utalii.

### 1.5.1.29 Sera ya Jinsia ya Zanzibar (2016)

Sera inakusudia kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha wanapata fursa sawa katika umiliki wa rasilimali na kuweka mazingira bora ya uzalishaji katika shughuli za uvuvi, uwezeshaji wa wananchi katika matumizi sahihi ya rasilimali na mazingira ya pwani, ikiwemo kilimo cha mwani na mazao mengine ya baharini, huduma za usafirishaji wa baharini, mafuta na gesi, na utalii.

### 1.5.1.30 Sera ya Usalama Kazini ya Zanzibar (2017)

Sera inasisitiza kuwepo kwa mazingira ya kazi yaliyo safi, salama na ya kiafya kwa utekelezaji mzuri wa majukumu na kuinua uchumi wa Taifa.

### 1.5.1.31 Sera ya Ardhi ya Zanzibar (2018)

Sera inaimarisha matumizi endelevu ya ardhi kupitia mikakati ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za pwani na mwambao.

#### 1.5.1.32 Sera ya Michezo ya Zanzibar (2018)

Sera inakuza ushiriki wa huduma za jamii kwenye maeneo ya utamaduni, burudani na michezo ya baharini na ufukweni kwa maendeleo ya Taifa.

#### 1.5.1.33 Sera ya Utalii ya Zanzibar (2018)

Sera inaimarisha utalii endelevu kwa kutilia mkazo utunzaji au uhifadhi wa urithi asilia na wa kiutamaduni unaozingatia matakwa muhimu ya kutunza mazingira.

#### 1.5.1.34 Sera ya Viwanda ya Zanzibar (2019)

Sera inaimarisha na kukuza ufahamu kuhusu umuhimu wa matumizi endelevu ya viwanda vya kati, vikiwemo viwanda vya sekta ya uvuvi, kwa maendeleo ya Taifa .

#### 1.5.1.35 Mkakati wa Zanzibar wa Utekelezaji wa Miongozo ya Shirika la Kimataifa la Safari za Baharini - IMO (2019)

Mkakati unalenga katika kuboresha viwango vya ulinzi na usalama kwa watu, vyombo vya majini, mali pamoja na taratibu za usimamizi wa viwango hivyo, sanjari na kuboresha mazingira ya kazi na haki zao za msingi.

#### 1.5.1.36 Mpango wa Dharura wa Zanzibar katika Kudhibiti na Kuzuia Umwagikaji Mafuta (2019)

Mpango huu unaelekeza njia za kudhibiti na kuzuia umwagikaji mafuta pamoja na kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya baharini. Vipaumbele vinavyozingatiwa ni pamoja na uhifadhii wa mazingira, usalama wa vyombo vya baharini, pamoja na wafanyakazi.

#### 1.5.1.37 Mkakati Jumuishi wa Zanzibar wa Usimamizi wa Taka Ngumu (2019)

Mkakati umeweka viwango vya usimamizi na udhibiti wa taka ngumu ili kupunguza uchafuzi wa mazingira ya maeneo ya baharini, ufukweni na mwambao dhidi ya kemikali zenye sumu na upotevu wa maji.

#### 1.5.1.38 Sera ya Biashara Ndogo na za Kati (SME) ya Zanzibar (2020)

Sera imeweka mazingira wezeshi ya uwekezaji wa biashara ndogo na za kati (SME) ili kuongeza kiwango cha uzalishaji na mapato. Sera inaelekeza kuongeza fursa za ajira kwenye shughuli za uvuvi, upatikanaji wa rasilimali na stadi mbalimbali katika kukuza uzalishaji, huduma za kifedha/mitaji, masoko, ongezeko la thamani ya mazao ghafi na kuwa na mfumo endelevu wa uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini.

#### 1.5.1.39 Sera ya Uwezeshaji ya Zanzibar (2022)

Sera inaimarisha uwezeshaji wa wananchi katika kujiendeleza kiuchumi na kujitegemea kwa azma ya kuinua kiwango cha uzalishaji, upatikanaji wa masoko, na tija.



# SURA YA PILI
# HALI HALISI

## 2.1 UTANGULIZI

Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa vidogo vidogo takriban 50 vilivyopo masafa ya kilomita 35 mashariki ya mwambao wa Tanzania Bara. Kisiwa cha Unguja ambacho ndio kikubwa chao kina eneo la kilomita za mraba 1,666, kikifuatiwa na Pemba chenye eneo la kilomita za mraba 988. Zanzibar ina eneo la ufukwe la kilomita za mraba 880, na kilomita za mraba 4,000 za eneo la pwani ambalo hutumiwa zaidi na wavuvi wadogo. Kisiwa cha Unguja kimeundwa kwa miamba ya matumbawe wakati cha Pemba ni miamba ya asili ya bara. Visiwa vyote vimezungukwa na miamba, fukwe za mchanga, wangwa , mikoko na matumbawe. Zanzibar inakadiriwa kuwa na wakaazi 1,889,773, wakiongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.7 kila mwaka (Sensa ya Watu, 2022).

*Zanzibar ina eneo la ufukwe la kilomita za mraba 880, na 4,000 za eneo la pwani*

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mamlaka kamili ya uhifadhi na usimamizi wa shughuli za uvuvi na maliasili za bahari katika maeneo yake ya maji ya ndani na ya kitaifa. Maji ya kitaifa ni bahari isiyopindukia masafa ya meli kumi na mbili kutoka maji ya ndani au mwambao wa visiwa vya Zanzibar.

Shughuli za uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini zina mchango mkubwa katika kendeleza ustawi wa jamii na uchumi wa Zanzibar. Umuhimu wa sekta ya uvuvi katika kuchangia uchumi wa Taifa na kutoa fursa za ajira, unatambuliwa na Sera na mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021-2026), Sera ya Uchumi wa Buluu ya Zanzibar (2022), na Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025). Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita (2020-2021) sekta ya uvuvi imepata mafanikio makubwa katika uzalishaji na ufanisi, na inachukuliwa kama kigezo cha kustawisha uchumi. Pamoja na mafanikio hayo, mwelekeo wa sasa ni kuweka mazingira bora ya kimkakati, kisera, na kisheria, ili kukabiliana na changamoto zilizopo na kufikia malengo ya maendeleo ya sekta ya uvuvi.

## 2.2 USIMAMIZI WA UVUVI

Sekta ya Uvuvi inatambulika katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 kama mchangiaji mkubwa katika uchumi wa taifa, kimapato, ajira na uhakika wa chakula.

Takribani shughuli zote za uvuvi mdogo mdogo zinazofanyika katika maji ya ndani na ya Kitaifa ya Zanzibar ni za kiwango kidogo, ingawa huvuliwa samaki wa aina mbalimbali, wengi wao wakiwa wa aina ya jodari, changu, pweza, na jamii ya samaki wanaoishi kwenye miamba ya matumbawe. Uvuvi wa kibiashara ambao unafanyika kwenye maji ya kina kirefu na eneo la bahari kuu unahusisha matumizi ya mishipi mirefu, na nyavu za kukokoteza.

Takwimu za sensa ya - uvuvi - (2020), zinaonesha kuwa Zanzibar ina jumla ya wavuvi 50,218 (ambapo asilimia 86 ni wanaume na asilimia 14 ni wanawake). Aidha, takribani watu 14,000 wanajishughulisha na shughuli mbali mbali zinazohusiana na uvuvi wa kiasili ikiwemo matengenezo na ukarabati wa zana na vyombo vya uvuvi; kuchakata na kusindika samaki, pamoja na huduma za masoko. Wavuvi wanatumia zana na vyombo vya asili kama vile mitumbwi, ngalawa mashua, na boti zenye mashine. Kati ya vyombo vya uvuvi 7,919 vilivyorikodiwa asilimia 43 vinatumia mashine.

*Zanzibar ina wavuvi 50,218, wanaume wakiwa 86% na wanawake 14%*

Pamoja na faida kubwa katika ukuzaji wa uchumi, sekta ya uvuvi ina umuhimu wa kipekee kwani ni chanzo kikuu cha upatikanaji wa protini ya asili ya wanyama. Wastani wa matumizi ya samaki kwa kila mtu kwa mwaka ni kilo 23, kiwango ambacho ni mara mbili zaidi ya wastani wa bara la Afrika wa kilo 9.4 kwa kila mtu kwa mwaka.

Takwimu za wastani wa uzalishaji wa samaki umeendelea kuongezeka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Uzalishaji mdogo unahusishwa na kutokuwepo kwa usimamizi na udhibiti wa kutosha dhidi ya matumizi ya vifaa, zana na mbinu za uvuvi zilizopigwa marufuku; na wavuvi wengi kurundikana kwenye eneo moja kwa sababu wanakosa mbinu na uwezo wa kuvua katika maji makubwa na eneo la bahari kuu. Hivyo pana-

hitajika usimamizi na udhibiti madhubuti utakaoongoza vyema matumizi endelevu ya rasilimali za bahari . Ni dhahiri kuwa mfumo wa usimamizi uliopo hauwezi kuharakisha mageuzi ya kisekta katika kutimiza majukumu ya kudhibiti, kuongoza, na kusimamia mazingira ya bahari na bayoanuai zake.

Kwa ujumla , upatikanaji wa samaki upo chini ya kiwango cha uzalishaji. Kwenye maji ya ndani na ya Kitaifa, matumizi ya vyombo vidogo vya uvuvi yamechangia katika kudumaza maendeleo ya shughuli za uvuvi na ufinyu wa fursa za ajira. Hali hii imepelekea uchafuzi wa mazingira na ekolojia ya maeneo ya pwani; ilhali eneo la maji ya kina kirefu na bahari kuu halijafikiwa na wavuvi wetu. Shughuli za uvuvi wa bahari kuu zinafanyika kwenye Ukanda Maalum wa Uchumi (EEZ) wa kilomita za mraba 223,000 chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu (DSFA) ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tokea mwaka 2009. DSFA ina mamlaka ya kisheria ya kuratibu uwekezaji katika shughuli za uvuvi katika ukanda maalum wa uchumi (kati ya maili 12 na 200 za baharini kutoka pwani). Uwekezaji huu ni fursa muhimu ya upatikanaji wa ajira kwa wavuvi na wasindikaji, kupatikana kwa fedha za kigeni (kutokana na mauzo ya bidhaa za uvuvi), na mapato ya Serikali kupitia mikataba ya uvuvi na kodi. Mchango mkubwa wa upatikanaji wa fursa za ajira upo katika shughuli za kusarifu samaki. Kwa mantiki hiyo, uwekezaji katika eneo la EEZ utawezesha matumizi ya vyombo, vifaa na mbinu za uvuvi wa kisasa, pamoja na wepesi wa ufuatiliaji na usimamizi.

Zanzibar, ikiwa sehemu ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, imeshiriki katika kutengeneza mfumo madhubuti wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi (MCS) chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) ili kuendesha shughuli za uvuvi katika ukanda wa EEZ. Mamlaka inafanya kazi zake kwa ushirikiano wa karibu na mashirika Pamoja na taasisi nyingine za umma ikiwemo Shirika la Meli na Uwakala la Tanzania (TASAC), Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ya Zanzibar (ZMA), Mamlaka za Bandari ya Tanzania Bara, Kikosi cha wanamaji cha Jeshi la Polisi, Kikosi cha wanamaji cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo cha Zanzibar (KMKM), na taasisi nyengine za sekta binafsi. Sheria na Kanuni zinazoongoza utendaji wa DSFA zinaelekeza kuwepo kwa ukaguzi wa vyombo vya uvuvi na doria za angani na baharini ili kuhakikisha kuwa vyombo vya uvuvi vinatekeleza masharti ya leseni. Majukumu makuu ya Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi (MCS) ni pamoja na kuratibu ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo vya uvuvi baharini; ukaguzi wa vyombo vya uvuvi; kufanya doria za baharini, angani na ufukweni; kufuatilia mwenendo wa ufungaji nanga na kuegesha kwenye madiko/bandari; uwekaji wa alama mahsusi kwenye vyombo na vifaa na zana za uvuvi ili kurahisisha ufuatiliaji, pamoja na utaratibu wa utoaji wa taarifa zinazohitajika kwenye kila chombo cha uvuvi.

*Shughuli za uvuvi wa bahari kuu zinafanyika kwenye Ukanda Maalum wa Uchumi (EEZ) wa kilomita za mraba 223,000 chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu*

Pamoja na kasi kubwa ya maendeleo ya kiuchumi kutokana na mazingira mazuri ya mageuzi ya kiuchumi na sera, sekta ya uvuvi ya Zanzibar bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalamu wenye uzoefu, pamoja na vitendea kazi ambavyo havikidhi mahitaji. Upungufu huu unachangia kuzorotesha utekelezaji na usimamizi wa sheria, kanuni na mikakati ya sera za uvuvi. Hivyo, ni muhimu kujenga uwezo wa kitaasisi katika masuala ya uendeshaji, usimamizi,ukaguzi pamoja na upatikanaji wa wataalamu wa kutosha.

*Majukumu makuu ya Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi (MCS) ni pamoja na kuratibu ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo vya uvuvi baharini*

Sekta ya uvuvi Zanzibar inakabiliwa na changamoto za Uvuvi haramu, Usioripotiwa na Usiodhibitiwa (IUU). Hali hiyo inahusishwa zaidi na uwezo duni warasilimali za ufuatiliaji bora, pamoja na udhibiti . Hivyo, mfumo imara na madhubuti katika maeneo ya hifadhi ya bahari wenye zana na teknolojia za kisasa unahitajika. Kulingana na taarifa ya FAO, Uvuvi haramu Usioripotiwa na Usiodhibitiwa unafanyika kwenye maeneo yote yauvuvi, kuanzia kwenye bahari kuu na maeneo ya udhibiti wa kitaifa.

Zanzibar pia haina taasisi zinazohusika na kutoa elimu katika fani ya kuendeleza na kuhifadhi rasilimali za baharini na maeneo ya pwani kwenye ngazi mbali mbali za ufundi, vyeti, stashahada na elimu ya juu. Ingawa mafanikio makubwa yamepatikana katika kujenga uwezo wa Kamati za Uvuvi za Shehia (SFCs) ngazi ya jamii, katika kuimarisha utoaji elimu, juu ya masuala ya uhifadhi na usimamizi wa maeneo tengefu,hasa katika Maeneo ya Hifadhi za Bahari (MCAs).

Katika ngazi ya kitaifa, bado hakuna jumuia za wavuvi na wadau wengine wa shughuli zinazohusiana na uvuvi. Usimamizi shirikishi unahitajika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sheria za uvuvi na kuenea kwa elimu ya uhifadhi wa mazingira. Aidha, kuna haja ya mfumo wa utayarishaji na utekelezaji jumuishi wa mpango mkuu wa usimamizi kwa kila eneo la uhifadhi wa bahari kwa ajili kulinda na kuhifadhi mazingira, na raslimali za baharini na ukanda wa pwani.

## 2.3 MAENDELEO YA KILIMO CHA MAZAO YA BAHARINI

Kilimo cha mazao ya baharini kinajumuisha shughuli za upandaji wa mwani, ufugaji wa samaki, kaa, matango bahari pamoja na viumbe vyengine vya baharini. Kilimo cha mazao ya baharini kinachangia kwa kiasi kikubwa kwenye mapato yatokanayo na uvuvi wa kienyeji. Shughuli kubwa zaidi miongoni mwao ni kilimo cha mwani, ambacho kimenyanyua ustawi wa maelfu ya wanawake katika jamii za pwani.  Takwimu za 2021 zinaonesha kwamba mwani ni miongoni mwa mazao makuu ya kibiashara kwa Zanzibar, ambapo jumla ya tani 12,000 zilisafirishwa nje ya nchi, zikiwa na thamani ya TZS 7,129,466,395 (OCGS, 2021).

Kutokana na kuongezeka kwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya pwani kulikopelekea kupungua samaki kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya miamba na matumbawe, shughuli za ufugaji wa samaki na kilimo cha mazao ya baharini zinazidi kushika kasi ili kukidhi mahitaji ya chakula na kuongezeka kwa fursa za ajira. Mbali na ukulima wa mwani, shughuli nyengine za ufugaji wa mazao ya baharini bado zipo kwenye hatua za awali. Miongoni mwa mazao ya baharini yanayoweza kufugwa vizuri hapa Zanzibar ni pamoja na samaki wa aina ya mwatiko, kolekole, mikizi, jamii ya kamba, matango bahari na kaa. Yapo maeneo mengi yenye mazingira wezeshi ya ufugaji kulingana na aina ya samaki na mfumo wa ufugaji, kupitia ujenzi wa mabwawa na vizimba. Ili kuendeleza shughuli za ufugaji wa mazao ya baharini, Serikali imejenga kituo cha uzalishaji wa vifaranga vya samaki, matango bahari, na kaa, pamoja na kuimarisha huduma za upatikanaji wa pembejeo za uzalishaji.

*Takwimu za 2021 zinaonesha kwamba mwani ni miongoni mwa mazao makuu ya kibiashara kwa Zanzibar*

*Kwa mujibu wa sensa ya hivi karibuni, mwani unalimwa na wakulima 23,000 ambapo kati yao asilimia 72 wako Pemba*

Ukulima wa mwani hapa Zanzibar ulianzishwa tokea miongo mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa sensa ya hivi karibuni, mwani unalimwa na wakulima 23,000 ambapo kati yao asilimia 72 wako Pemba. Asilimia 80 ya wakulima wa mwani wa Zanzibar ni wanawake. Mwani umekuwa chanzo mbadala cha mapato kwa jamii za pwani. Kwenye maeneo kadhaa wanawake wamejisajili kwenye vikundi vya ushirika na kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa mwani ambapo wanazalisha na kuuza bidhaa mbali mbali kama vile sabuni, mafuta,vipodozi, madawa, vyakula na vinywaji.

Changamoto zinazojitokeza ni pamoja na maambukizi ya maradhi ya aina tofauti, hujuma za wadudu na vimelea, pamoja na kiwango kidogo cha bei ya ununuaji wa mwani kulinganisha na uzito wa huduma za uzalishaji. Aina mbili kuu za mwani zinazolimwa ni mwani mwembamba (*Eucheuma denticulatum*) ambao pia hujulikana kama spinosum, na aina ya cottonii mwani



mnene (*Kappaphycus alvarezii*). Mwani wa spinosum ndio unaolimwa na kustawi zaidi, ingawa bei yake kwenye soko ipo chini kuliko mwani wa cottonii. Changamoto nyengine ni upatikanaji mdogo wa pembejeo za uzalishaji, zinazopelekea wakulima kuokota mbegu zisizo na ubora kutoka maeneo ya pwani. Kadhalika, yapo matatizo ya utaalamu mdogo wa uzalishaji miongoni mwa wakulima, hujuma za wizi, na masuala mengine yanayohusiana na usalama mdogo katika mashamba ya wanajamii. Aidha, ongezeko la uwekezaji wa shughuli za kiutalii katika maeneo ya fukwe unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwanyima wazalishaji fursa ya kuyafikia na kuyatumia maeneo yao ya uzalishaji.

Maendeleo ya ufugaji wa samaki na kilimo cha mazao ya baharini (ukuzaji wa viumbe maji) yanaathiriwa kwa kiasi kikubwa na utaalamu mdogo wa kuendesha biashara, upatikanaji mdogo wa mitaji pamoja na kukosekana



kwa taarifa za masoko. Hivyo kuna haja kwa sekta binafsi kukuza biashara na mazingira ya uwekezaji kwa wakulima wadogo wadogo kusudi waweze kuongeza thamani kwenye bidhaa wanazozalisha, pamoja na kuendeleza au kuanzisha vyama na vikundi vya kuweka na kukopa. Kadhalika, kutokuwepo kwa mwongozo wa usimamizi jumuishi miongoni mwa taasisi za Serikali kunadumaza lengo la kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa raslimali za bahari kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

## 2.4 ULINZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA BAHARINI

Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MCAs) ndani ya Zanzibar ni mifumo muhimu ya kiikolojia katika kutunza mazingira ya bahari, uboreshaji wa maeneo ya mazalia na ukuaji wa samaki, mimea na viumbe vyengine vya baharini, pamoja na shughuli za utalii. Jumla ya maeneo matano ya hifadhi za bahari yameanzishwa (Jadwali 2.1) zenye ukubwa wa eneo la takriban kilomita za mraba 2,161.7 ikilinganishwa na eneo lote la bahari ya ndani la Zanzibar lenye kilomita za mraba 2,350.

Jadwali 2.1: Maeneo ya hifadhi za Bahari ya Zanzibar.

| ENEO LA UHIFADHI | MWAKA WA USAJILI | ENEO (km$^2$) |
|---|---|---|
| Hifadhi ya Bahari ya Mkondo wa Pemba (PECCA) | 2005 | 825.8 |
| Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Menai (MBCA) | 1997 | 717.5 |
| Hifadhi ya Bahari ya Mnemba (MIMCA) | 2002 | 337.3 |
| Hifadhi ya Bahari ya Tumbatu (TUMCA) | 2014 | 162.9 |
| Hifadhi ya Bahari ya Changu-Bawe (CHABAMCA) | 2014 | 118.2 |

Kupitia mfumo wa usimamizi shirikishi, uhifadhi wa maeneo ya bahari unatoa fursa nyingi za kiuchumi na maendeleo ya jamii. Kila eneo limetayarishiwa mpango wake mkuu wa usimamizi. Hatahivyo, maslahi ya watumiaji wa baharini yanakinzana na mpango huo, hivyo kukwamisha usimamizi endelevu.

Miamba ya matumbawe ni maeneo muhimu ya mazalia, malishio ya samaki pamoja na ukuwaji wa viumbe kadhaa. Maeneo haya ni muhimu kwa uvuvi wa kienyeji ambao unanufaisha zaidi ya asilimia 45 ya shughuli za uvuvi. Katika miaka ya hivi karibuni, mahitaji ya rasilimali za uvuvi yameongezeka kwa kasi kubwa kutokana na ongezeko la idadi ya watu na kukua kwa shughuli za utalii. Hii imepelekea kuongezeka kwa matumizi ya vifaa, zana na mbinu za uvuvi haramu Pamoja na uchafuzi wa mazingira ya baharini. Aidha muendelezo wa uvuvi haramu, mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na athari za tabia ya nchi umepelekea uharibifu wa miamba ya matumbawe. Kwa mantiki hii, uboreshaji wa maeneo ya matumbawe unahitaji juhudi za ulinzi shirikishi wa wadau mbalimbali pamoja na mipango

ya usimamizi wa rasilimali endelevu ndani ya mfumo imara wa usimamizi wa ushirikiano.

Pamoja na umuhimu wa shughuli za uvuvi wa burudani, ambazo pia huitwa michezo ya baharini, ambayoinawezesha kukuza teknolojia ya uvuvi na kuimarisha huduma za utalii wa baharini, shughuli hizo muhimu bado hazijapewa uzito unaostahiki. Na kwa hakika fursa zinazotokana na michezo ya baharini haziwezi kupuuzwa. Hivyo, Sera ya Uvuvi ya Zanzibar na sheria zinazohusiana zitaendeleza wigo mpana wa uvuvi wa burudani ikiwa ni pamoja na uvuvi wa samaki wa mapambo.



Kuna aina kadhaa za viumbe bahari vilivyo hatarini kutoweka kwenye maeneo ya bahari ya Zanzibar, na ambao wana umuhimu mkubwa katika suala la uhifadhi wa viumbe hai na shughuli za utalii wa ikolojia. Miongoni mwao ni pamoja na pomboo, nyangumi, nguva, papa, makobe, na kasa. Aidha taarifa kamili za idadi na mazingira yao zinakosekana; na mifumo yao ya kuhama kutoka eneo moja hadi jengine bado haieleweki vizuri. Hizi ni miongoni mwa changamoto katika shughuli za uhifadhi endelevu wa viumbe adimu, na utafiti wa utalii wa baharini kwa viumbe adimu vilivyo hatarini kutoweka.

Mazao yanayopatikana katika maeneo ya miamba ya matumbawe kama vile jamii mbali mbali za samaki, makome, matango bahari, pweza, kamba, na chaza, yana mahitaji na manufaa makubwa kimataifa. Kwa mantiki hiyo, uhifadhi wa maeneo ya matumbawe ni njia ya kipekee ambayo inapaswa kuzingatia mambo kadhaa umakini, mambo hayo ni pamoja nakupiga marufuku biashara ya matumbawe, pamoja na biashara ya jamii zote za viumbe zilizo orodheshwa chini ya Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya Viumbe na Mimea ya Bahari Waliohatarini Kutoweka (CITES).

kwa ujumla, uwezo wa kiutendaji, kwa maana ya usimamizi wa shughuli za uvuvi, kwenye maeneo ya hifadhi ya bahari bado ni mdogo. Bado panahitajika mfumo jumuishi wa usimamizi wa maeneo ya baharini na pwani ili kuepusha migogoro ya kimatumizi. Sera itajumuisha mikakati ya Upangaji, Matumizi na Usimamizi wa Maeneo ya Bahari (MSP). mchakato ambao ni muhimu katika kupanga, kuchambua na kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi ya kwa shughuli za binadamu, ili kutumia vizuri rasilimali za baharini na kuhifadhi malengo ya kiikolojia, kiuchumi na kijamii. Kadhalika, maadili ya kitamaduni hayajaunganishwa kwa kiasi cha kutosha katika mfumo wa usimamizi, na upashanaji taarifa, na umiliki wa pamoja. Kwa ujumla, mfumo wa utawala unakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kusawazishwa.

## 2.5 UTAFITI NA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA BAHARINI

Utafiti wa kisayansi katika shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini umeongezeka duniani kote kwa kasi kubwa katika kipindi cha miaka 20 hadi 30 iliyopita. Utafiti huo unashinikizwa na haja ya kuendeleza utafiti wa ikolojia ya pwani, mfumo wa tathmini na ufuatiliaji, kufanya maamuzi ya uhifadhi na usimamizi wa shughuli za uvuvi kulingana na mbinu za uzalishaji, masuala ya tabia nchi, pamoja na udhibiti wa jamii ya viumbe na mimea bahari.

*Mwaka 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilianzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI)*

Kazi za utafiti wa uvuvi na mazao ya baharini hapa Zanzibar zilianza kushika kasi mwishoni mwa miaka ya 1970. Taasisi za awali katika kufanya utafiti zilikuwa ni Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) pamoja na Shirika la Utafiti wa Uvuvi wa Baharini la Afrika Mashariki (EAMFRO). Kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mwaka 1978, majukumu ya EAMFRO yalihamishiwa katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam (IMS). Shughuli za utafiti zilijumuisha utafiti uliozingatia biolojia ya uvuvi, matumbawe, mikoko na mazingira ya viumbe na mimea bahari, matumizi ya zana za uvuvi na uhifadhi wa maeneo ya bahari..

Katika juhudi za kuimarisha utafiti wa uvuvi, mwaka 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilianzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) ikiwa na mamlaka ya kuratibu na kusimamia utafiti wote wa uvuvi na rasilimali za bahari. Shughuli za utafiti zinalenga kuondoa changamoto zilizopo kufuatana na vipaumbele vya utafiti vilivyoainishwa kwenye Ajenda ya Utafiti (ZRA) kwa miaka 2021-2026 katika sekta ya uvuvi.

Kwa kiasi kikubwa shughuli za utafiti zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazohusiana na mifumo isiyo madhubuti ya kupata takwimu za aina ya samaki, wingi na mtawanyiko wa samaki, mazao ya baharini; pamoja na usambazaji wa taarifa sahihi na kwa wakati mwafaka. Ili kufanikisha uendeshaji wa tafiti zenye tija na matokeo Chanya, ni ukweli kwamba, kunahitajika fedha pamoja na rasilimali nyenginezo kutegemeana na aina ya utafiti. Uhaba wa rasilimali watu na fedha kumepelekea kuwa na viwango duni katika ukusanyaji, uhifadhi, utayarishaji wa takwimu, usambazaji wa teknolojia mpya, pamoja na matukio yanayohusika. Katika muda huu ambapo maambukizi ya magonjwa yanayohusiana na matumbawe kwenye pwani ya Zanzibar na Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIO) bado yapo kwenye kiwango cha chini, bado zipo dalili za uwezekano wa kuongezeka kwa matukio hayo. Ongezeko hili la maradhi pia linahusishwa na kuingizwa kwa jamii mpya za mimea na viumbe bahari kutoka maeneo yaliyoathirika.

Katika mazingira ya sasa ya kiutendaji, hakuna taasisi yenye miundombinu sahihi na uwezo wa kudhibiti ubora wa viwango vya mazao ya baharini. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwepo taasisi itakayohusika kuhakiki viwango na kuthibitisha ubora wa bidhaa zote za mazao ya baharini zinazoingizwa ndani na kusafirishwa nje ya Zanzibar.

Kwenye kilimo cha mwani, utafiti umezingatia zaidi masuala ya uzalishaji na mbinu bora za ukulima wa mwani mwembamba na mwani mnene.

## 2.6 UPATIKANAJI WA SOKO, ONGEZEKO LA THAMANI NA MIUNDOMBINU

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeazimia kuimarisha uvuvi endelevu, wa kibiashara na viwanda. Uwekezaji mkubwa utahusisha shughuli za uvuvi kwenye maji ya ndani ya kina kirefu, ya kitaifa na eneo la bahari kuu; pamoja na huduma za usindikaji wa mazao ya baharini. Usindikaji wa samaki unajumuisha shughuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kusarifu, kusafisha, , kuweka barafu, kukausha, kufungasha, kuweka chumvi, na njia nyingine kufuatana na mahitaji ya masoko. Mafanikio ya uwekezaji kwenye minyororo ya thamani yataipatia Zanzibar fursa ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini, na wakati huo huo kutosheleza soko la ndani na hivyo kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo nchini.

Miongoni mwa fursa za uvuvi wa bahari kuu ni uhakika wa kuvua na kuwasarifu samaki kwa masoko ya nje, ambapo aina mbali mbali za samaki kama vile jodari, sehewa, mbasi, changu, fatundu, sansuri, na wengineo wanapatikana kwa wingi.

Madiko ni vituo vya msingi katika utoaji wa huduma za awali za kusarifu, kuuza na kununua samaki wakiwa salama kiafya. Kwenye maeneo haya, kwa kawaida samaki huuzwa kwa njia ya mnada. Hata hivyo upungufu wa zana, vifaa na mitambo ya kuhifadhia mazao ya baharini kwenye maeneo ya madiko kunasababisha upotevu mkubwa wa ubora wa bidhaa. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo (FAO, 2012), Zanzibar



inakabiliwa na upotevu wa asilimia 25 ya bidhaa za samaki kwenye mnyororo wake wa thamani. Pamoja na mahitaji makubwa ya samaki kwenye soko la ndani, bado hakuna mazingira mazuri ya kibiashara kwa wavuvi, wachuuzi, madalali, wauzaji wadogo wadogo na wanunuzi. Aidha, ongezeko la kasi ya bei ya samaki linahusishwa na kupungua idadi ya samaki wanaovuliwa ikilinganishwa na kuongezeka kwa mahitaji, hasa kwenye sekta ya utalii.

Sehemu kubwa ya samaki wa jamii ya dagaa wanaovuliwa, hukaushwa moja kwa moja kwenye maeneo ya fukwe, na kisha kusafirishwa na wanunuzi kupitia kwa mawakala wao kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Juhudi za kuwawezesha wajasiariamali katika kuboresha ubora wa usindikaji na ufungashaji wa dagaa zimeanza kufanikiwa. Hata hivyo, masuala yanayohusiana na uhakika wa chakula na usafi wa mazingira kwenye maeneo ya fukwe bado yanahitaji kushughulikiwa. Mchango wa sekta ya uvuvi katika masoko ya nje ya nchi bado ni mdogo kutokana na sababu mbali mbali, ikiwamo mahitaji makubwa ya soko la ndani ikilinganishwa na kiwango cha uzalishaji. Aidha, ukosefu wa taasisi ya vipimo na viwango vya ubora inachangia kuongeza ugumu kufikia viwango vya kimataifa vya usafirishaji wa samaki na bidhaa zake. Katika kipindi hiki, takriban samaki na bidhaa zote za baharini zinauzwa zikiwa hazijachakatwa au kwa kiwango kidogo tu cha usarifu. Hali hii inatokana zaidi na uwekezaji mdogo kwenye matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuongeza uzalishaji wa tija kwenye sekta ya uvuvi.

Tafiti chache sana zimefanyika kwenye minyororo ya thamani ya mwani na ufugaji wa mazao ya baharini. Kwa upande wa mwani, mnyororo wake wa thamani unaishia kwenye usafirishaji wa mwani uliokaushwa, ambapo inakadiriwa kuwa mkulima anapata asilimia 0.26 ya bei ya soko la dunia. Kwa mazao mengineyo, mifumo ya mazingira wezeshi ya ufugaji, biashara na uwekezaji, inahitajika ili kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko.

Njia mojawapo muhimu ya kukabiliana na changamoto za kitaaluma, uchakataji, pamoja na kuongeza thamani, ni kuendanana mabadiliko ya sayansi na teknolojia zinazotumika katika sekta ya uvuvi. Wavuvi wetu wadogo wadogo bado wanashindwa kutumia fursa za kuvua kwenye maji ya kina kirefu kutokana na ukosefu wa mitaji, vyombo na utaalamu wa uvuvi wa viwanda. Kadhalika, Kiwango cha Juu cha Mavuno Endelevu (MSY), ambacho kinasaidia katika kutambua uhalisia wa matumizi ya maeneo ya bahari, bado hakijulikani, hususan kwenye maeneo ya pwani. Mazao yenye umuhimu kwenye masoko ya nje ya nchi kama vile makombe na matango bahari yameadimika na viwango vyao vya usafirishaji pia vimeshuka. Ubora wa bidhaa unaathiriwa na vifaa na vyombo duni vya uhifadhi, uchakataji na usafirishaji. Taratibu zinazohusiana na usafirishaji ni ngumu, zenye usumbufu, zinatumia muda mrefu kukamilisha na zinahusisha gharama nyingi za kifedha kutokana na milolongo ya kodi na ada kwenye mamlaka tofauti.

Mfumo wa usambazaji unatoa mwanya kwa madalali kununua bidhaa kwa bei nafuu na kuuza kwa bei kubwa. Hakuna miongozo wala taratibu za kitaasisi zinazosimamia masoko ya bidhaa za uvuvi. Aidha, hadi sasa hakuna taasisi yoyote yenye mamlaka ya kuhakiki viwango pamoja na kuthibitisha ubora wa bidhaa zote za baharini zinazoingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi. Kadhalika, hakuna unafuu wa upatikanaji wa huduma, vifaa pamoja na pembejeo za uvuvi kwa wavuvi wadogo wadogo. Taarifa za mwenendo wa soko



la nje la mwani zinakosekana, huku ukiritimba ukidhibiti masoko yake ya ndani.

Kuna haja ya kuendeleza mabadiliko ya sekta ya uvuvi na kuifanya kuwa ya uzalishaji wa kibiashara na ushindani. Ni muhimu kubadilisha mtizamo na mawazo ya wadau, kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, kuimarisha ubora na uhakiki wa viwango, pamoja na kuimarisha mifumo na miundombinu ya soko la ndani, kikanda na kimataifa.

## 2.7 HOJA MTAMBUKA

Sekta ya Uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini imeajiri watu 79,856 ambapo asilimia 29 ni wanawake. Angalau asilimia 62.89 ya waajiriwa ni wavuvi, ambapo asilimia 14 miongoni mwao ni wanawake. Kilimo cha mwani kinachangia asilimia 19.86 ya ajira ambayo kati yao asilimia 74 ni wanawake. Hivyo wanawake wana mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini.

Kwa wakazi wengi wa mwambao, shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini ndio chanzo kikuu cha mapato na uwepo wa uhakika wa chakula. Wengi wao ni wanyonge na wenye kipato cha chini, kwa sababu maisha yao ya kila siku yanategemea shughuli za uvuvi mdogomdogo na kwa kiasi fulani kilimo duni cha kutumia jembe la mkono, pamoja na kukosa haki katika umiliki wa rasilimali. Pia hawana uwezo na fursa za kutetea haki zao. Hali hii ambayo hailingani na utajiri wa asili wa pwani wala hailingani na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya pwani, inahitaji kuwekewa mikakati itakayowahusisha wadau wote kujibidisha kuyahifadhi mazingira kwa uzalishaji zaidi kwa manufaa yao ya kijinsia, kijamii na kiuchumi. Sera ya Uchumi wa Buluu ya 2022 inatambua na kusisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii wakiwemo vijana, wazee, na watu wenye mahitaji maalumu katika kuwanasua katika janga la umasikini linalowakabili. Kadhalika, Mkakati wa Kuboresha Utawala na Usimamizi wa Uvuvi wa mwaka 2014, umeelekeza katika kukuza masuala ya jinsia na kuwapa kipaumbele watumiaji wa raslimali za uvuvi. Mkakati umeshauri kuwepo juhudi za kutosha za kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na uvuvi katika kuongeza kipato cha wadau hususan wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum.

Kama ilivyo kwa Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo (SIDS), Zanzibar inakabiliwa na hatari ya kupungua eneo lake la ardhi kutokana na kupanda kwa kina cha bahari, ongezeko la idadi ya wakaazi, na uharibifu wa rasilimali zake kutokana na utegemezi mkubwa wa rasilimali za bahari kwa kupata mahitaji muhimu ya kijamii na kiuchumi. Mabadiliko ya tabia nchi pamoja na shughuli za kibinaadamu yamesababisha madhara makubwa yakiwemo kuongezeka kwa joto la bahari, kuathiri uwezo na uhimilivu wa maeneo ya fukwe na mazingira ya baharini, hali inayopelekea matokeo mabaya ya kijamii na kiuchumi. Mabadiliko ya hali ya hewa yanapelekea kuongezeka kwa kiwango cha joto, kuongezeka kwa majanga ya asili kama vile mafuriko, mmon'gonyoko wa fukwe na kuingia kwa maji ya bahari, kupungua kwa idadi ya mimea na viumbe bahari, kupungua kwa kiwango cha maji ardhini na kusababisha kuongezeka kwa kiwango cha maji ya chumvi. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na udhibiti mzuri dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya kimaumbile imetayarisha mpango endelevu wa matumizi bora ya maeneo ya pwani kupitia mkakati wa mabadiliko ya tabia ya nchi wa mwaka 2014, pamoja na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa 2021 uliotoa mwongozo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kukosekana kwa taarifa za uhakiki wa viwango vya mazingira hatarishi kwenye maeneo mbali mbali, ni vigumu kutayarisha na kuandaa mikakati ya kukabiliana na dharura mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za tahadhari. Mbali na gharama kubwa, faida zake pia hazionekani moja kwa moja. Kwa maana hiyo, Sera itakuwa na mikakati ya kupambana na uhalifu katika shughuli za uvuvi pamoja na magendo kupitia kujenga uwezo wa watumishi na upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi. Zanzibar bado haina uzoefu wa kutosha kwenye masuala ya uwekekezaji kwenye huduma za ulinzi na kinga kupitia sekta binafsi. Aidha uwezo wa taasisi za serikali katika kusimamia mazingira hatarishi haujakomaa. Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mwanachama kupitia mikataba, itifaki na mazimio ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia. Changamoto kubwa ni kuimarisha uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu katika utekelezaji wake.

# SURA YA TATU
# DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA

## 3.1 UTANGULIZI

Zanzibar inalenga kukuza shughuli endelevu za uvuvi ili kukidhi mahitaji ya ndani na usafirishaji nje ya nchi kwa ajili ya kuimarisha uchumi pamoja na kuinua mchango wa sekta ya uvuvi kwenye Pato la Taifa, kama ilivyo-elekezwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Ili shughuli za uvuvi ziwe endelevu, inapaswa kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, mifumo ya kijamii, kiuchumi pamoja na maslahi ya watu. Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) unaelekeza katika kui-nua kiwango cha uzalishaji na uboreshaji wa viwango kwa bidhaa za uvuvi, mazao ya baharini pamoja na rasilimali nyenginezo kwa lengo la kuwawezesha wavuvi na wakulima wa mazao ya baharini kuwekeza kwenye uvuvi wa kisasa.

## 3.2 DIRA NA DHAMIRA YA SERA

**Dira**

> *'Uvuvi wenye kustawisha na kuongoza kwa ufanisi na tija kwenye sekta ya uchumi wa buluu utakaopelekea kuboresha viwango vya kijamii na kiuchumi vya Wazanzibari, na ukuaji wa Pato la Taifa*

**Dhamira**

> *Kufanikisha maendeleo ya mipango endelevu ya uvuvi kupitia usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za baharini, uimarishaji wa miundombinu ya kuongeza thamani, ustawi wa jamii, pamoja na uhifadhi endelevu wa mazingira na kujikinga dhidi ya mabadiliko ya tabianchi*

## 3.3 MALENGO YA SERA

Lengo kuu la Sera ya Uvuvi ya Zanzibar ni kukuza maendeleo endelevu ya Sekta ya Uvuvi.

Malengo mahsusi ni:

1. Kuimarisha utendaji wa sekta ya Uvuvi kupitia mipango bora ya uvuvi inayokidhi mahitaji ya wadau wa uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini.
2. Kukuza shughuli za uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini kwa kutumia teknolojia za kisasa.
3. Kuimarisha usimamizi wa mazingira kwa kud-hibiti, kuongoza na kusimamia mazingira na bayoanuai na ekolojia ya bahari.
4. Kukuza teknolojia katika utafiti, ugunduzi na ubunifu uvuvi na sayansi ya bahari ili kufungua fursa za uchumi wa buluu.
5. Kuendeleza minyororo ya thamani ya mazao ya uvuvi kwa kupunguza upotevu wa mavuno, kui-marisha viwango vya usalama na usafi, usarifu na masoko, pamoja na huduma za miundombinu ili kukidhi masoko ya kimataifa.
6. Kuimarisha uhakika wa chakula na lishe katika ngazi ya familia kupitia usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi; na
7. Kuimarisha ushiriki na upatikanaji wa fursa sawa kwa wanajamii kwa kujenga uwezo wa vijana, wanawake, na watu wenye mahitaji maalum.



## 3.4 MISINGI ELEKEZI

Misingi inayosimamia na kuiongoza Sera ya Uvuvi pamoja na utekelezaji wake inaendana na vipaumbele vya kitaifa vifuatavyo:

1. Uendelevu: Sera inaelekeza katika kuepusha athari hasi za kijamii, kiuchumi na kimazingira;
2. Uhifadhi: Sera inalenga katika uhifadhi na usimamizi endelevu wa bahari na ukanda wa pwani;
3. Utafiti: Sera inakusudia kukuza utafiti na maendeleo wa rasimali za bahari ;
4. Kupunguza umaskini: Matumizi endelevu ya rasimilai za Bahari katika kupunguza umasikini.
5. Usawa wa Kijinsia: Sera inaelekeza kutoa huduma kwa njia ya uwazi na usawa bila ya ubaguzi wa kijinsia kwa wanaume, wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum.
6. Ushirikiano na Sekta binafsi: Kupanga na kutekeleza mipango ya sekta ya uvuvi kwa njia ya ubia kati ya mashirikiano ya sekta ya umma na binafsi katika.
7. Usimamizi Shirikishi: Sera inatilia mkazo katika usimamizi shirikishi unaowahusisha wanajamii, mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), taasisi ziziso za kiserikali (NGOs), taasisi za kijamii (CBOs), mashirika ya umma, taasisi za sekta binafsi, washirika wa maendeleo, na vikundi vya uhifadhi wa mazingira.
8. Huduma za Ugani: Sera inaweka mkazo katika kujenga uwezo wadau wa sekta ya uvuvi, taasisi binafsi na za kijamii kupitia ushajiishaji, uhamasishaji, na utoaji wa mafunzo maalum ili kukuza kiwango cha uwekezaji wa sekta ya uvuvi.
9. Ufuatiliaji, Udhibiti na Ufuatiliaji katika usimamizi wa uvuvi: Sera inasisitiza kufanya tathmini ya udhibiti na ufuatiliaji kwa ufanisi na uwazi ili kulinda maslahi ya sekta ya uvuvi.
10. Uwazi na uwajibikaji: Sera inahakikisha kusimamia misingi ya utawala bora katika kukuza uwazi na uwajibikaji.
11. Uwezeshaji: Sera inasisitiza juu ya ushiriki na uwezeshaji wa wadau mbali mbali wa sekta ya uvuvi wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum kwa kuwapatia stadi na mitaji ya uwekezaji katika minyororo ya thamani ya sekta ya uvuvi.
12. Ushindani: Sera inalenga kuhakikisha ushindani wa haki katika sekta ya uvuvi ili kuongeza masilahi ya jamii.
13. Uwajibikaji wa jamii: Sera inashajihisha uwajibikaji wa jamii na watendaji.
14. Utawala bora: Sera itakuza na kuimarisha misingi ya utawala bora katika utekelezaji wake.



# SURA YA NNE
# HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

## 4.1 UTANGULIZI

Sera ya Uvuvi ya Zanzibar inasimamia maeneo sita ya kimkakati, ambayo yamechambuliwa kwa mujibu wa hoja na matamko ya kisera pamoja na mikakati yake ya utekelezaji kama ifuatavyo:

## 4.2 USIMAMIZI WA UVUVI

### 4.2.1 UWEZO WA KITAASISI

**Hoja ya Kisera**: Usimamizi mzuri wa sekta ya uvuvi unakwamishwa na uwezo mdogo wa kitaasisi, kiteknolojia, rasilimali watu na kifedha; hivyo kusabaisha udhaifu mkubwa katika utekelezaji na usimamizi wa sheria na sera zinazohusiana na shughuli za uvuvi. Wakati mabadiliko ya kiuchumi yamejenga mazingira mazuri ya maendeleo ya haraka ya kiuchumi, bado kuna upungufu wa wataalamu wenye uzoefu na ujuzi kwenye fani mbali mbali za sekta ya uvuvi. Zanzibar pia inahitaji uwepo wa vyuo na taasisi muhimu za kuzalisha wataalamu kwa ajili ya sekta hii. Aidha, bado hakuna jumuia za wavuvi na nyenginezo zinazohusiana na shughuli za uvuvi katika ngazi ya kitaifa.

**Tamko la Sera**: Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, itaimarisha uwezo wa sekta ya uvuvi kitaasisi, kiteknolojia, kifedha na rasilimali watu.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha taasisi za usimamizi wa sekta ya uvuvi ili kutoa huduma bora;
2. Kuwekeza katika ajira na maendeleo ya rasilimali watu.
3. Kuanzisha taasisi ya umma na kudumisha miundombinu ya mafunzo katika fani ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini;
4. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika teknolojia ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini, pamoja na taasisi za mafunzo.
5. Kuboresha mifumo ya ushirikishwaji wa wadau ili kuimarisha maendeleo ya sekta ya uvuvi;
6. Kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa wavuvi na wakulima wa mazao ya baharini;
7. Kuhimiza uanzishwaji wa mifumo ya bima katika sekta ya Uvuvi;
8. Kukuza na kuunga mkono uanzishaji wa vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa vinavyohusiana na uvuvi; na
9. Kuanzisha na kusimamia mfuko maalum wa maendeleo ya sekta ya uvuvi.

### 4.2.2 USIMAMIZI JUMUISHI

**Hoja ya Kisera**: Usimamizi jumuishi uliopo haukidhi ufanisi katika kusimamia sheria na kueneza elimu ya uhifadhi wa mazingira. Aidha, jamii haina uwezo wa kiteknolojia, na shughuli zao za uvuvi zinaishia kwenye maji ya ndani na katika maji ya kina kidogo. Hii inapelekea sekta ya uvuvi kuzalisha chini ya uwezo wake halisi. Mfumo huu wa uvuvi unaathiriwa na ufinyu wa mifumo ya utafiti, usambazaji wa elimu, pamoja na uhaba wa wataalamu. Zaidi ya hayo, kuna ukosefu wa upatikanaji wa taarifa muhimu juu ya masuala yanayohusiana na huduma za mikopo, bei za bidhaa, hali ya masoko, uhifadhi baada ya kuvuna, pamoja na viwango vya ubora na usalama kwa bidhaa za uvuvi.

**Tamko la Sera**: serikali itaimarisha ushirikishwaji wa jamii katika sekta ya uvuvi ili kuweka misingi imara ya ufuatiliaji, udhibiti na ukaguzi, pamoja na kuibua fursa za ubunifu katika kuendeleza na kukuza teknolojia na kushiriki katika ufanyaji wa maamuzi.

**Mikakati ya Utekelezaji** :

1. Kuimarisha usimamizi shirikishi wa jamii katika kufanya maamuzi ya busara ya usimamizi na uvunaji wa raslimali za uvuvi pamoja na uhifadhi wa mazingira.
2. Kukuza maswala ya jinsia na kuwapa kipaumbele wadau au watumiaji wa raslimali za uvuvi katika kupanga, kutoa maamuzi na utekelezaji katika ngazi zote.

3. Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika kuwezesha matumizi ya teknolojia wezeshi kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija.
4. Kuimarisha uundaji wa vyama vya ushirika vya uvuvi na ukulima wa mazao ya baharini ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma.
5. Kutayarisha na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa kutokana na usimamizi shirikishi ili kufanikisha upeanaji wa habari na taarifa ulio thabiti;
6. Kutetea na kushawishi ushiriki wa jamii katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuhakikisha kwamba taasisi za usimamizi wa uvuvi zinapokea na kusambaza taarifa kwa umma kwa wakati stahiki.
7. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika upatikanaji wa njia mbadala za kuongezea kipato ili kupunguza wimbi la uvunaji wa raslimali za bahari.

### 4.2.3 UWEKEZAJI NA MITAJI

**Hoja ya Kisera**: Hakuna mitaji ya kutosha ya kuwezesha uwekezaji, pamoja na kuwepo fursa kubwa ya kuwekeza katika viwanda vya kusarifu samaki na mazao ya baharini. Vilevile mifumo ya mageuzi ya kuibadilisha sekta ya uvuvi kutoka uvuvi wa kujikimu na kuwa wa kibiashara na wenye ushindani bado haijawa timilifu.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha uwekezaji wa uvuvi wa kibiashara ili kunyanyua fursa za ujenzi wa viwanda vya kusarifu bidhaa za samaki ili kuongeza thamani kwenye mazao ya uvuvi kwa misingi ya kukuza uchumi na masoko.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha uwekezaji katika uvuvi wa kibiashara na viwanda vyake vya usarifu;
2. Kuwezesha ujenzi wa bandari za uvuvi na madiko; na
3. Kuunga mkono mageuzi ya uvuvi mdogo mdogo kuelekea uvuvi wa kibiashara.

### 4.2.4 UZALISHAJI WENYE TIJA

**Hoja ya Kisera**: Kiwango cha uzalishaji wa samaki pamoja na tija kinazidi kuporomoka. Uvuvi haramu nao umeendelea kuharibu ekolojia ya bahari na kuathiri uzajilishaji wa samaki wenye tija. Aidha, tatizo la ukosefu wa pembejeo na huduma za ugani, ukosefu wa mitaji na wataalamu ambao unakwaza uvuvi wa bahari kuu. Vile vile, teknolojia za kisayansi zinazotumika katika kuelewa kiwango cha juu cha mavuno (MSY) ni dhaifu. Aidha, Zanzibar bado haijatumia vyema fursa za kiuchumi zitokanazo na uvuvi wa bahari kuu na ukanda maalum wa uchumi wa bahari. Maarifa na utaalamu wa asili unashajiisha katika ulinzi na uhifadhi endelevu wa rasilimali za baharini na ukanda wa pwani. Maarifa haya ni muhimu na yanapaswa kutumika katika usimamizi endelevu wa sekta ya uvuvi.

**Tamko la Sera**: Serikali itakuza shughuli za uvuvi wa kibiashara na kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kutumia maarifa na utaalamu endelevu wa kijadi na wenye tija unaounganishwa na matumizi ya vyombo vya uvuvi wa viwanda ili kuongeza fursa za ajira zenye staha.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

Kuendeleza na kusimamia mpango wa matumizi ya matumbawe bandia (FAD);

1. Kuimarisha maendeleo ya jumuia za wavuvi kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa kuwekeza kwenye uvuvi wa kisasa;
2. Kuendeleza wavuvi wazawa katika uvuvi wa bahari kuu ambao unalenga samaki aina ya jodari na jamii yake;
3. Kuhamasisha taasisi za fedha ili kutoa huduma za upatikanaji wa pembejeo na mikopo nafuu kwa wavuvi wadogo na wakulima wa mazao ya baharini;
4. Kuendeleza mafunzo ya shughuli za uvuvi na maonyesho ya vitendo ili kukuza kasi ya uwasilishaji na matumizi ya teknonolojia kwa wepesi;
5. Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na utafiti ili kuelewa kiwango halisi na aina ya samaki wanaovuliwa;
6. Kulinda na kushajiisha matumizi ya maarifa na utaalamu wa jadi ili kuimarisha uvuvi endelevu; na
7. Kuhifadhi maeneo muhimu ya mazalia, malishio na ukuwaji wa viumbe na mimea ya baharini ili kuimarisha upatikanaji endelevu wa rasilimali za baharini.

### 4.2.5 UFUATILIAJI, UDHIBITI NA UKAGUZI (MCS)

**Hoja ya Kisera**: Mfumo wa sasa wa Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi unakwamishwa na upungufu wa watumishi wenye ujuzi na vifaa vya kutendea kazi. Maeneo ya uvuvi yaliyo mbali hayafikiki kwa urahisi, idadi ya wavuvi inaongezeka kwa kasi, na maeneo mengi ya uvuvi bado yanahitaji mfumo madhubuti wa ufuatiliaji, udhibiti na ukaguzi. Aidha uvuvi wa kurundikana kwenye eneo la maji ya ndani, pamoja na kutotii sheria na kanuni za usimamizi dhidi ya uvuvi haramu, vinapunguza kiwango cha uzalishaji.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha uwezo wa kufanya kazi za ufuatiliaji, udhibiti na ukaguzi ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni za simamizi na udhibiti wa sekta ya uvuvi.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuwekeza kwenye kuimarisha uwezo wa rasilmali watu kwenye eneo la Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi;
2. Kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa Ufuatiliaji, Udhibiti na.Ukaguzi kwa kuweka vifaa na vitendea kazi vya kutosheleza; na
3. Kufanya mapitio ya sheria na kanuni za uvuvi.

**Hoja ya Kisera**: Sekta ya Uvuvi inaathiriwa na uvuvi haramu, usioripotiwa na usiodhibitiwa (IUU), unaohusishwa na utekelezaji dhaifu katika usimamizi wa Sheria na Kanuni za uvuvi pamoja na uratibu usiofaa katika kuwasimamia wavuvi wadogo wadogo kwenye maeneo ya uvuvi.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha uwezo wa kitaalamu wa sekta ya uvuvi pamoja na utoaji wa zana na vifaa vya kisasa, uhamasishaji wa wavuvi wadogo wadogo, pamoja na kukuza ushirikiano wa kikanda

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuongeza uelewa na kujenga uwezo kwa wavuvi na jamii inayowazunguka
2. Kuimarisha uwezo wa rasilmali watu kwenye eneo la Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi;
3. Kufanya mapitio na kutekeleza sheria na kanuni za uvuvi.
4. Kutekeleza doria ya anga na bahari.
5. Kuimarisha uhusiano wa kitaifa na kikanda

## 4.3 MAENDELEO YA KILIMO CHA MAZAO YA BAHARINI

### 4.3.1 USIMAMIZI WA KILIMO CHA MAZAO YA BAHARINI

**Hoja ya Kisera**: Usimamizi kwenye kilimo cha mazao ya baharini unakabiliwa na changamoto za kiutawala kutokana na sera zenye kukinzana. Vile vile ipo migogoro baina ya wavuvi, kwa mfano, maeneo ya ukulima na ukaushaji wa mwani pia ndiyo maeneo ya wavuvi kupitisha na kuegesha vyombo vyao, na maeneo hayo hayo ndiyo yanayotumika kwa shughuli za utalii na kusababisha eneo la ufukwe kudhibitiwa na wamiliki wa hoteli. Changamoto nyengine ni matatizo ya afya yanayotokana na shughuli za uzalishaji wa mazao ya baharini, pamoja na maradhi ya zao la mwani. Fursa za uwekezaji kwenye kilimo cha mazao ya baharini bado hazijaibuliwa kikamilifu. Kwa hivyo Serikali itahamasisha ushiriki wa sekta binafsi na jamii kuwekeza kwenye kilimo cha mazao ya baharini.

**Tamko la Sera**:Serikali itaimarisha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa shughuli za kilimo cha mazao ya baharini ili kuratibu ushiriki mkubwa wa wadau, kutatua migogoro ya matumizi ya rasilimali, kuimarisha afya, na kuongeza fursa za ajira zenye staha.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuandaa na kutekeleza mifumo ya utaratibu kwa ajili ya kuimarisha utawala bora na utatuzi wa migogoro;
2. Kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa hali ya afya ya wazalishaji, na ya viumbe na mimea ya baharini;
3. Kuimarisha shughuli za kilimo cha mazao ya baharini kwa washiriki mbali mbali kwenye minyororo yote ya thamani;
4. Kuihamasisha jamii kuwekeza katika shughuli za kilimo cha mazao ya baharini kwenye maeneo ya mwambao;

5. Kukuza ushirikiano na sekta binafsi katika uwekezaji wa kilimo cha mazao ya baharini kwenye maeneo ya mwambao;
6. Kukuza uwezo wa wazalishaji wa mazao ya baharini katika upatikanaji wa vifaranga na kuwaunganisha na vituo vya uzalishaji na ukuzaji wa vifaranga.

### 4.3.2 TEKNOLOJIA KATIKA MAZAO YA BAHARINI

**Hoja ya Kisera**: Changamoto katika kilimo cha mazao ya baharini zinahusishwa na uwezo mdogo wa teknolojia ya uzalishaji, uongezekaji mdogo wa thamani kwa bidhaa za mazao ya baharini, ujuzi na utaalamu mdogo wa biashara na upatikanaji mdogo wa soko.

**Tamko la Sera**: Serikali itakuza na kudhibiti ubunifu na matumizi ya teknolojia kwa maendeleo ya kilimo cha mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kukuza na kuimarisha uwezo wa usimamizi bora wenye ujuzi wa kutosha kwenye teknolojia za uzalishaji, shughuli za kilimo na usimamizi wa biashara ya mazao ya baharini, teknolojia za uhifadhi wa mazao, na masoko ya bidhaa za mazao ya baharini.
2. Kuimarisha matumizi ya ujuzi wa kienyeji ili kukuza uenezi wa habari kwa wadau mbalimbali; na
3. Kukuza matumizi ya utaalamu wa asili na upashanaji mzuri wa habari miongoni mwa wadau mbalimbali;
4. Kuweka na kuimarisha mazingira mazuri ya uwekezaji katika matumizi ya teknolojia sahihi za kilimo cha mazao ya baharini na maendeleo ya teknolojia.

### 4.3.3 PEMBEJEO ZA MAZAO YA BAHARINI

**Hoja ya Kisera**: Ukosefu wa pembejeo bora unakwaza maendeleo ya kilimo cha mazao ya baharini hapa Zanzibar. Aidha matatizo ya upatikanaji wa pembejeo yanapelekea wakulima wa mazao ya baharini kutafuta mbegu dhaifu kutoka kwenye maeneo yasiyo rasmi.

**Tamko la Sera**: serikali itashajiisha na kuunga mkono juhudi za sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa pembejeo bora, kuimarisha huduma za kitaalamu na mitaji ya kuanzisha uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza tasnia ya kilimo cha mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kushajiisha na kuunga mkono juhudi za sekta binafsi katika upatikanaji wa mbegu bora, chakula na pembejeo nyenginezo;
2. Kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo cha mazao ya baharini; na
3. Kuunga mkono juhudi za wadau katika kutoa huduma na unafuu wa upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo cha mazao ya baharini.

## 4.4 ULINZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA BAHARI

### 4.4.1 UHIFADHI WA RASILIMALI ZA BAHARI

**Hoja ya Kisera**: Uwezo wa kulinda na kuhifadhi rasilimali za baharini bado ni mdogo. Idadi kubwa ya jamii ya samaki wa kwenye miamba ya matumbawe wako hatarini kutoweka, na mazingira ya maisha yao bado hayaeleweki vizuri. Hivyo hatua zinafaa kuchukuliwa ili kuweka mazingira mazuri kwa kuimarisha shughuli za uvuvi wa burudani, pamoja na kudhibiti uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira. Hali hii inahitaji ushirikano wa wadau mbali mbali kupitia mfumo wa usimamizi shirikishi.

**Tamko la Sera**:Serikali itaimarisha uwezo wa kisekta katika kusimamia maeneo ya hifadhi ya baharini kwa kubuni mbinu mwafaka na matumizi sahihi ya zana za uvuvi, utalii wa baharini ikiwa pamoja na uvuvi wa burudani ndani ya maeneo ya hifadhi ili kudhibiti uharibifu, kurejesha mazingira halisi ya miamba na matumbawe, pamoja na kuhifadhi viwango vya mazingira.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kufanya mapitio na kutekeleza mpango mkuu wa usimamizi wa maeneo ya uhifadhi wa baharini, makumbusho ya baharini na maeneo tengefu kwa ajili ya kuimarisha huduma za uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya baharini;
2. Kushajiisha matumizi sahihi ya zana na vifaa vya uvuvi katika maeneo ya uhifadhi wa baharini.

3. Kuimarisha uvuvi wa burudani ikiwemo uvuvi wa kitalii na michezo ya baharini;
4. Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kufadhili na uwezeshaji wa jamii kwenye kusimamia na kuhifadhi rasilimali za baharini;
5. Kutayarisha na kutekeleza mpango maalum wa kusimamia na kulinda viumbe adimu na vilivyo hatarini kutoweka;
6. Kuwezesha mwenendo wa samaki wenye tabia ya kuhama kutoka eneo moja hadi jengine kupitia uhifadhi na usimamizi wa maeneo tengefu;
7. Kuimarisha huduma za usalama wa maisha na afya za wavuvi;
8. Kuimarisha mipango ya bima ya maisha kwa wavuvi.

### 4.4.2 MIPANGO YA RASILIMALI ZA BAHARI

**Hoja ya Kisera**:Mfumo madhubuti wa ushirikishwaji katika usimamizi na uhifadhi katika ukanda wa pwani unahitajika ili kuepusha migogoro pamoja na kuimarisha uhifadhi wa rasilimali. Taarifa ziliopo za kiekolojia pekee hazitoshi, hasa katika masuala ya utandawazi wa rasilimali za mazao ya baharini na ambazo hupelekea kuvunwa kwa njia zisizo endelevu. Kuna haja pia ya kuimarisha mila na utamaduni, ulinzi wa maeneo ya kihistoria, na ulinzi shirikishi katika maeneo ya uhifadhi na usimamizi.

**Tamko la Sera**: Serikali itawezesha ulinzi shirikishi katika ukanda wa pwani ili kuimarisha usimamizi na uhifadhi endelevu wa mazingira ya bahari na bayoanuai.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kufanya mapitio na kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uhifadhi wa ukanda wa pwani (ICZM);
2. Kutayarisha na kutekeleza programu za kuielimisha na kuiwezesha jamii katika uhifadhi wa mazingira;
3. Kuanzisha, kutekeleza na kuratibu mipango shirikishi ya usimamizi na uhifadhi wa ukanda wa pwani; na
4. Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maeneo ya uhifadhi katika kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi ya rasilimali za baharini.

### 4.4.3 MIPANGO YA MATUMIZI YA MAENEO BAHARINI (MSP)

**Hoja ya Kisera**: Mahitaji ya rasilimali za baharini yanaongezeka kwa kasi, kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na kukuwa kwa sekta ya utalii. Migogoro katika matumizi ya bahari miongoni mwa wadau mbali mbali inaendelea kuathiri juhudi za usimamizi na hifadhi ya rasilimali za baharini. Utekelezaji wa sheria ni legelege na haufanyi kazi katika kudhibiti rasilimali. Upungufu wa rasilimali za bahari katika maeneo kadhaa huwashawashi wavuvi kuhamia maeneo mengine na kusababisha migogoro miongoni mwa wavuvi.

**Tamko la Sera**: Serikali itawezesha Upangaji wa Matumizi wa Maeneo ya Bahari kwa upatikanaji wa taarifa muhimu zinazohitajika katika mchakato wa kupanga, kuchambua na kutenga matumizi ya rasilimali za baharini na kuhifadhi malengo ya kiikolojia, kiuchumi na kijamii.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha juhudi za uhamasishaji, kujenga uwezo wa kiufundi na usimamizi, pamoja na utaalamu wa ukusanyaji wa taarifa za sekta ya uvuvi;
2. Kufanya mashauriano na utafiti wa kina katika ukusanyaji wa taarifa za sekta ya uvuvi kwa ajili ya Upangaji wa Matumizi wa Maeneo ya Bahari; na
3. Kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Upangaji wa Matumizi wa Maeneo ya Bahari.

## 4.5 TAFITI KWA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA BAHARI

### 4.5.1 TEKNOLOJIA NA KUJENGA UWEZO

**Hoja ya Kisera**: Bado hatujawa na uwezo wa kutosha katika medani ya utafiti kwa maendeleo utaotuwezesha kufanya maamuzi sahihi katika maeneo ya uvuvi, mazao ya baharini, sayansi ya bahari, pamoja na utafiti katika maji ya ndani, maji ya taifa na ukanda maalum wa uchumi. Vile vile lipo tatizo la upungufu wa wataalamu, vitendea kazi, pamoja na rasilimali fedha. Aidha, uwezo mdogo katika ukusanyaji wa takwimu, kufanya uchambuzi na tathmini pamoja na kutayarisha ripoti unaathiri mfumo mzima wa utayarishaji wa

taarifa za kitaalamu ambazo ni muhimu katika kufanya maamuzi sahihi kuhusu usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za baharini.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha uwezo wa utafiti kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi kwa ajili upatikanaji wa taarifa sahihi za usimamizi wa kisekta.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha shughuli za utafiti kwa maendeleo kwenye sekta ya uvuvi ili kukidhi malengo ya sasa na ya baadae;
2. Kuimarisha mfumo wa kanzidata ya taarifa, kumbukumbu na usimamizi wa sekta ya uvuvi.
3. Kushawishi kuanzishwa kwa programu maalum za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini katika mfumo wa elimu wa kitaifa;
4. Kufanya tathmini za kuelewa kiwango, aina na mgawanyiko wa samaki; na
5. Kushirikiana na taasisi zinazotambulika katika masuala ya utafiti.

### 4.5.2 FEDHA ZA UTAFITI

**Hoja ya Kisera**: Ukosefu wa fedha za kutosha unakwamisha juhudi za utafiti katika sekta ya uvuvi hadi kuonekana kama ni jambo la kawaida tu. Shughuli za utafiti wa maambukizi ya maradhi kwenye pwani ya Zanzibar na Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIO) zinafanyika kwa kiwango kidogo sana. Zaidi ya hayo, takwimu kwa ujumla wake zinaonesha ongezeko dogo la samaki wanaovuliwa. Kwa kiasi kikubwa shughuli za utafiti zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazohusiana na mifumo duni ya kupata takwimu za aina, wingi na mtawanyiko wa samaki na mazao ya baharini; pamoja na usambazaji wa taarifa sahihi na kwa wakati mwafaka. Bila shaka kuendesha utafiti kunahitaji fedha nyingi na rasilimali nyenginezo ili kuweza kufanya kazi yenye matokeo mazuri. Uhaba wa rasilimali watu na fedha kumepelekea kuwa na viwango duni katika ukusanyaji, uhifadhi, utayarishaji wa takwimu na usambazaji wa teknolojia mpya, pamoja na matukio yanayohusika. Katika muda huu ambapo maambukizi ya magonjwa yanayohusiana na matumbawe kwenye pwani ya Zanzibar na Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIO) bado yapo kwenye kiwango cha chini, kuna dalili za kuongezeka kwa matukio hayo. Ongezeko hili la maradhi pia linahusishwa na kuingizwa kwa jamii mpya za mimea na viumbe bahari kutoka maeneo yaliyoathirika.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha na kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia ufadhili wa kuwezesha kufanyika utafiti kwenye maeneo yaliyopewa kipaumbele.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuweka ubia katika utafiti kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi;
2. Kuimarisha mbinu bunifu za ufadhili na upatikanaji wa fedha ili kuendeleza utafiti katika ngazi zote za sekta ya uvuvi;
3. Kuendeleza ubia na ushirikiano na taasisi za elimu ya juu pamoja na taasisi nyenginezo za utafiti.

### 4.5.3 MFUMO WA USIMAMIZI WA TAARIFA ZA SEKTA YA UVUVI

**Hoja ya Kisera**: Mfumo wa sasa wa usimamizi wa taarifa za shughuli za uvuvi haukidhi mahitaji ya sekta ya uvuvi. Taarifa za usimamizi zinahitajika kuwa kwenye kiwango bora na kuwekwa kwenye mfumo wa ki-elektronic wa Serikali Mtandao kupitia mifumo ya ufuatiliaji ya shughuli za uvuvi na ikolojia ya baharini.

**Tamko la Sera**: Serikali itaendeleza mifumo itakayosaidia katika kujenga misingi imara ya ufuatiliaji na tathmini kwenye shughuli za uvuvi na ekolojia ya baharini katika maeneo ya Ufuatiliaji, Udhibiti na Ukaguzi; sambamba na uratibu wa takwimu, utoaji wa leseni, pamoja na hali ya masoko.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha mfumo wa habari za masoko ya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini;
2. Kuunganisha mifumo ya upashanaji habari kwenye maeneo ya tahadhari ya mapema, na usimamizi wa leseni;
3. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji, udhibiti na ukaguzi;
4. Kujenga uwezo katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za sekta ya uvuvi; na

5. Kuunganisha mifumo ya uhakiki wa ubora na uthibitishaji wa bidhaa katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za sekta ya uvuvi.

## 4.6 UPATIKANAJI WA MASOKO, ONGEZEKO LA THAMANI, MIUNDOMBINU, UDHIBITI WA UBORA NA VIWANGO

### 4.6.1 HUDUMA ZA UPATIKANAJI WA MASOKO

**Hoja ya Kisera**: Kwa sasa, mifumo ya masoko na ujasiriamali inayohusiana na uvuvi mdogo mdogo bado haitumiki kikamilifu kwa sababu ya mifumo duni ya uuzaji wa bidhaa. Taarifa za upatikanaji wa soko hazipatikani kwa wakati na kwa uhakika. Mfumo wa usambazaji wa bidhaa unatoa mwanya kwa madalali kununua bidhaa kwa bei nafuu na kuuza kwa bei kubwa kutokana na kutokuwepo kwa miongozo, kanuni, wala taratibu za kitaasisi zinazosimamia masoko ya bidhaa za uvuvi.

**Tamko la Sera**: Serikali itaboresha mifumo ya masoko na uhusiano wa bidhaa za uvuvi ili kuimarisha uwazi katika huduma za upatikanaji wa soko.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuwezesha mazingira rafiki ya kuwezesha sekta binafsi kufanya biashara za shughuli za uvuvi;
2. Kuimarisha miundombinu ya masoko na mawasiliano ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwenye masoko;
3. Kukuza na kuimarisha uwezo wa uzalishaji na mauzo ya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini kwa njia endelevu;
4. Kurahisisha taratibu za usafirishaji ili kukuza usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi; na
5. Kutafuta na kuunganisha masoko la kikanda na kimataifa.

### 4.6.2 ONGEZEKO LA THAMANI

**Hoja ya Kisera**: Uongezaji wa thamani na uuzaji wa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini kwa sasa unafanyika kwa kiwango kidogo. Tunashindwa kuzitumia fursa mpya za kibiashara kutokana na viwango duni vya usindikaji ambavyo havikidhi mahitaji ya soko. Usindikaji unafanyika katika kiwango kidogo sana, na sehemu kubwa ya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini zinaingia sokoni bila kusarifiwa. Vifaa na vyombo vya uhifadhi, uchakataji na usafirishaji bado havitoshelezi. Sambamba na hayo mfumo wa kuhakiki ubora wa viwango kwa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini unahitaji kuimarishwa.

**Tamko la Sera**: Serikali itakuza matumizi ya teknolojia bora katika usafirishaji, usindikaji, uhifadhi, usarifu na kuongeza thamani kwa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji** :

1. Kushajiisha na kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya usindikaji wa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini;
2. Kuendeleza uwekezaji katika uongezaji wa thamani kwa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini;
3. Kukuza matumizi ya mitambo ya kisasa ya kusarifu na kufunganisha bidhaa
4. Kuimarisha huduma za uhifadhi na udhibiti wa bidhaa za uvuvi; na
5. Kuimarisha uwezo wa wajasiriamali wadogo wadogo kuwekeza katika uongezaji wa thamani kwa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini;

### 4.6.3 MIUNDOMBINU

**Hoja ya Kisera**: Ukosefu wa miundombinu mizuri kwenye maeneo ya madiko, masoko na sehemu za kuhifadhia samaki unachangia sana katika upotevu wa samaki na mazao ya baharini. Tunahitaji pia kuzikabili changamoto za uhaba wa wataalamu, sambamba na matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuongeza thamani bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini. Aidha, kutokana na matatizo ya umiliki wa ardhi, maeneo ya madiko yanabadilishwa na kutumika kwa kazi nyengine, ikiwemo ujenzi wa hoteli za kitalii.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha udhibiti, umiliki na uwekezaji katika madiko, bandari za uvuvi, na miundombinu ya masoko, pamoja na kuweka vifaa na vyombo vya uchakataji, kusarifu na uhifadhi.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kukuza uwekezaji kwenye bandari za uvuvi, madiko, na miundombinu ya soko kwa kuimarisha huduma za usarifu na uhifadhi;

2. Kutayarisha utaratibu wa motisha wa kuwavutia wawekezaji;
3. Kuimarisha udhibiti na umiliki, ikiwa pamoja na upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo yote ya madiko; na
4. Kushiriki katika kufanya tathmini za kubaini, kuendeleza na kurasimisha maeneo ya kambi za uvuvi na madiko.

### 4.6.4 UDHIBITI WA UBORA NA VIWANGO

**Hoja ya Kisera**: Ubora na viwango vya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini ni duni kutokana na kutokuwepo kwa ufanisi katika udhibiti wa ubora, ithibati, pamoja na mifumo ya usimamamizi. Hali hii inaathiri sana usalama wa chakula na usafi wa mazingira. Aidha, inahitajika mamlaka yenye uwezo wa kusimamia uhakiki wa ubora na uthibitishaji wa bidhaa zote za uvuvi na mazao ya baharini.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha na kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika uhakiki wa ubora na uthibitishaji wa bidhaa zote za uvuvi na mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuanzisha na kuwezesha Mamlaka ya uhakiki wa ubora na uthibitishaji wa bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini zinazoingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi.
2. Kutayarisha na kusimamia viwango vya uhakiki wa ubora na uthibitishaji wa bidhaa;
3. Kuanzisha viwanda vya kusarifu bidhaa za uvuvi;
4. Kushirikiana na maabara ya kitaifa kwenye mfumo wa uidhinishaji na uthibitishaji wa ubora na viwango vya bidhaa za uvuvi na mazao ya baharini;
5. Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa ithibati wa ubora na viwango vya bidhaa za uvuvi; na.
6. Kutengeneza na kutekeleza muundo wa kujenga uwezo wa wataalamu wa sekta ya uvuvi kufuatana na minyororo yake ya thamani; na
7. Kuimarisha miundo mbinu ya uhifadhi na usafirishaji.

## 4.7 HOJA MTAMBUKA

### 4.7.1 KUATHIRIKA NA UHIMILIVU WA MABADILIKO YA TABIA NCHI

**Hoja ya Kisera**: Kama ilivyo kwa Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo (SIDS), Zanzibar inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kupanda kwa kina cha maji ya bahari kutokana na udogo wa eneo lake, ongezeko la idadi ya watu na utegemezi mkubwa wa maliasili kwa ajili ya kupata chakula na mahitaji mengine. Vilevile ongezeko la joto na kiwango cha chumvi baharini na eneo la pwani vinaathiri mazingira ya bahari, uharibifu wa miamba ya matumbawe, kutoweka kwa mikoko pamoja na kuathirika maeneo ya mazalia na malisho ya samaki. Aidha, kutokana na kukosekana kwa taarifa za uhakiki wa viwango vya mazingira hatarishi kwenye maeneo mbali mbali, ni vigumu kutayarisha na kuandaa mikakati ya kukabiliana na dharura mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za tahadhari. Uwezo wa taasisi za serikali katika kusimamia mazingira hatarishi haujakomaa.

**Tamko la Sera**: Serikali itaandaa utaratibu mzuri wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya matumizi endelevu ya sekta ya uvuvi.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kushiriki katika kuimarisha miradi ya kitaifa ya kukabiliana na kudhibiti ongezeko la hewa ukaa ili kupunguza uchafuzi wa hewa na ongezeko la joto duniani;
2. Kujumuisha taaluma ya kisayansi, ushirikiano wa kiufundi, na uwezo wa shughuli za utafiti katika teknolojia ya uvuvi, kilimo cha mazao ya baharini pamoja na sayansi ya baharini na hali ya hewa;
3. Kuimarisha uwezo na ushiriki kwenye kusimamia miongozo sheria, na kanuni za sekta ya uvuvi katika kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.
4. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika kuhifadhi bioanuwai ya mimea na wanyama bahari kupitia utekelezaji wa program ya Ahuweni ya UVIKO-19; na
5. Kuimarisha usimamizi wa mazingira na uhifadhi wa bioanuai.

### 4.7.2 UWEZESHAJI WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE MAHITAJI MAALUM

**Hoja ya Kisera**: Ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika sekta ya uvuvi hauridhishi. Hivyo ujumuishaji wa kijinsia na uchambuzi wa minyororo ya thamani ni muhimu sana katika kutayarisha mikakati ya uwezeshaji wa jamii za wavuvi, watu wasio na uwezo na usawa wa kijinsia, wakiwemo miongoni mwao wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha ujumuishaji wa kijinsia kwa usimamizi endelevu wa shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini, kwa kuweka mkazo zaidi katika uhamasishaji wa jamii, ubunifu, miundombinu, mitaji na masoko.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha uwezo wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum kuwekeza kwenye miradi ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini;
2. Kuimarisha uwepo wa huduma za soko kwa wanawake, vijana, na watu wenye mahitaji maalum kwenye miradi ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini;
3. Kuimarisha ulinzi kwa wanawake, vijana, na watu wenye mahitaji maalum kwenye miradi ya sekta ya uvuvi.
4. Kujumuisha na kuunganisha fursa zote za ajira zenye staha zinazoambatana na shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini katika upangaji wa mikakati, programu na miradi; na
5. Kuhamasisha jamii za wavuvi hasa wanawake na vijana katika kujikinga na maradhi ya kuambukiza.

### 4.7.3 MARADHI YA KUAMBUKIZA

**Hoja ya Kisera**: Jamii za wavuvi wa Zanzibar wanakabiliwa na hatari za maradhi ya kuambukiza katika kazi zao za uvuvi.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha huduma za mazingira rafiki kwenye maeneo ya uvuvi kwa ajili ya kukinga jamii za wavuvi dhidi ya maradhi ya kuambukiza.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha uelewa wa elimu ya afya ya jamii na kujenga uwezo wa wanajamii kukabiliana na dharura mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za tahadhari;
2. Kushirikiana na taasisi za afya katika kuielimisha jamii kuelewa, kukinga na kudhibiti maradhi ya kuambukiza;
3. Kushawishi kupitia taasisi mbali mbali usimamizi wa huduma za usafi na afya ya jamii kwenye maeneo ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini;
4. Kuzipatia kambi za dago vifaa na miundombinu ya huduma ya afya na ustawi wa jamii;
5. Kuwakinga wanawake, vijana na makundi maalum dhidi ya matumizi wa madawa ya kulevya na udhalilishaji.

### 4.7.4 RASILIMALI MBADALA ZA UZALISHAJI

**Hoja ya Kisera**: Idadi kubwa ya wavuvi na wakulima wa mazao ya baharini wa Zanzibar wanategemea shughuli za uvuvi mdogomdogo, na hawana njia mbadala wala uwezo wa kutosha wa kujikwamua kimaisha. Ni dhahiri kuwa zipo fursa mbali mbali za kiuchumi ambazo zinahitaji kuwekewa mikakati ya uzalishaji itakayowahusisha wadau wote kujibidisha katika kuyahifadhi mazingira kwa uzalishaji zaidi kwa manufaa yao ya kijinsia, kijamii na kiuchumi.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha na kuwezesha upatikanaji wa fursa mbali mbali za kiuchumi katika sekta ya uvuvi ili kunyanyua hali ya maisha ya jamii za wavuvi na wakulima wa mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuhamasisha utamaduni wa ujasiriamali miongoni mwa jamii za wavuvi;
2. Kuimarisha mikakati ya kiuchumi kwa kwa jamii za wavuvi katika miradi ya kijamii na utoaji wa huduma;
3. Kuimarisha upatikanaji wa haki na usawa kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi na kilimomazao ya baharini, ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa miradi midogo midogo; na
4. Kushirikiana na sekta binafsi na taasisi za ustawi wa jamii katika kuimarisha ajira zenye staha na ustawi wa jamii.

### 4.7.5 UTULIVU NA USALAMA WA BAHARINI

**Hoja ya Kisera**: Ipo haja kubwa ya kufanya mapitio ya sheria ziliopo kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia utekekelezaji wa kanuni na miongozo katika kulinda na kuboresha mazingira ya haki, maslahi na ustawi wa mabaharia. Mkazo zaidi unapaswa kuelekezwa kwenye kuyakabili masuala ya uhalifu wa baharini sambamba na kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema ili kujikinga na majanga.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha mazingira ya utulivu na usalama wa baharini kwenye shughuli za uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini.

**Mikakati ya Utekelezaji**

1. Kushajiisha jamii katika masuala ya kuimarisha usalama wa baharini;
2. Kuimarisha ushirikiano, katika ngazi zote, na taasisi mbali mbali kwenye masuala ya utulivu na usalama wa baharini;
3. Kushiriki katika kusimamia utekekelezaji wa sheria na kuimarisha uwezo wa taasisi zenye dhamana ya ufuatiliaji katika sekta ya uvuvi;
4. Kushiriki katika kuanzisha taasisi za taaluma ya baharini, vituo vya uokozi, na vituo vya kuongoza vyombo vya baharini;
5. Kuimarisha utayari wa kukabiliana na maafa ya baharini kupitia mikakati stahiki ya kukinga na kuhimili maafa, sambamba na mifumo ya tahadhari ya mapema; na
6. Kujumuisha hasara zitokanazo na maafa na mifumo ya bima.

### 4.7.6 USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA

**Hoja ya Kisera**: Changamoto muhimu kwa Zanzibar ni kuimarisha uwezo wa kukabili kasi ya mabadiliko katika utekelezaji wa mikataba, itifaki na maazimio ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwenye sekta ya uvuvi. Hivyo upo umuhimu mkubwa wa kuimarisha ushirikiano katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa ili kufanikisha utekelezaji wa sera ya uvuvi kwa lengo la kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na mazao ya baharini.

**Tamko la Sera**: Serikali itaimarisha uwezo wa kukabili kasi ya mabadiliko ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa ufanisi.

**Mikakati ya Utekelezaji**:

1. Kuimarisha ushirikiano wa wadau mbali mbali katika kupanga na kutekeleza mipango ya sekta ya uvuvi;
2. Kuimarisha ushiriki wa uwezeshaji wa serikali za mitaa kutekeleza miradi ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini;
3. Kuimarisha ushiriki na uwezeshaji wa wadau mbali mbali wa sekta ya uvuvi kwa njia ya uwazi na usawa bila ya ubaguzi wa kijinsia kwa wanaume, wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum; na
4. Kushiriki katika vikao, hafla, makongomano, na mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa.

# SURA YA TANO
# MFUMO WA KISHERIA NA KITAASISI WA SERA

Kwa kuzingatia wigo mpana wa sekta ya uvuvi, ni muhimu kuwa na mfumo madhubuti wa uratibu wa sera na sheria ili kuchochea mabadiliko jumuishi katika maendeleo ya uchumi wa viwanda, sayansi na teknolojia kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa kitaasisi na sheria, sanjari sambamba na utekelezaji wa maazimio, mikataba, itifaki na makubaliano ya kikanda na kimataifa katika sekta ya uvuvi.

## 5.1 MFUMO WA KITAASISI

Utekelezaji wa sera ya uvuvi hii utasimamiwa na taasisi zinazohusika na shughuli za uvuvi ,na ufugaji kilimo na ukulima wa mazao ya baharini chini ya Wizara yenye dhamana ya uvuvi. Taasisi hizo ni Idara zinazohusika na maendeleo ya uvuvi, uhifadhi wa rasilimali za baharini, pamoja na utafiti wa uvuvi na rasilimalimaliasili za baharini. Vilevile sera hii itatekelezwa kwa ushirikiano miongoni mwa Taasisi za Serikali, Taasisi zisizo za Serikali, Pamoja na wadau wengine wa sekta hii mbali mbali kama ifuatavyo:

## 5.2 MFUMO WA KISHERIA

Wizara yenye dhamana ya uvuvi itaongoza utekelezaji wa sera ya uvuvi hii kwa kutunga na kufanya mapitio ya sheria za sekta ya uvuvi. Hii itajumuisha kufanya mapitio ya Sheria ya uvuvi ya mwaka 2010, kutunga sheria ya Uhifadhi wa Bahari, pamoja na sheria ya taasisi ya utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini.

## 5.3 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WASHIRIKI WAKUU WA SERA

Utekelezaji wa sera ya uvuvi hii ni unajumuisha Wizara zote za Serikali, Sekta binafsi, Asasi za kiraia na Wadau wa maendeleo.

### 5.3.1 WIZARA YENYE DHAMANA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

1. Kusimamia Kuwa ni msimamizi mkuu wa utekelezaji wa sera ya uvuvi;
2. Kuhakikisha kuwepo kwa maendeleo endelevu katika sekta ya uvuvi;
3. Kuimarisha muundo wa utekelezaji wa sheria na kanuni za sekta ya uvuvi;
4. Kujenga uwezo wa kusimamia utekelezaji wa sera ya uvuvi wenye tija na ufanisi;
5. Kuweka mazingira rafiki ambayo yatatoa motisha ya kuwezesha matumizi ya teknolojia kwa wavuvi wadogo wadogo na wakulima wa mazao ya baharini.
6. Kuwezesha upatikanaji wa soko na ongezeko la thamani kwa mazao ya baharini.
7. Kujenga uwezo wa wawekezaji na wavuvi wadogo wadogo na wawekezaji wa ndani ili kuweza kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu;
8. Kulinda maslahi ya wavuvi na maeneo ya madiko katika kukabiliana na athari za uchumi jumuishi;
9. Kuwawezesha wawekezaji wa ndani wazawa kushiriki kwenye uwekezaji katika sekta ya uvuvi.kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi;
10. Kuiimarisha shughuli za utafiti na ufuatiliaji wa maendeleo ya sekta ya uvuvi; na
11. Kuwezesha kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika wa sekta ya uvuvi.

### 5.3.2 WIZARA YENYE DHAMANA YA FEDHA NA MIPANGO

1. Kutafuta na kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu za uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini;
2. Kuelekeza vigezo na masharti ya matumizi ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini;
3. Kuweka mazingira bora na utaratibu kwa wawekezaji wa ndani Kuwezesha mikataba na masharti nafuu ya uwekezaji;
4. Kurekebisha kanuni za fedha na manunuzi ili kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi;
5. Kuimarisha taasisi za fedha kwa ajili ya kujenga mazingira wezeshi ya uwekezaji wa biashara ndogo ndogo na za kati;

6. Kujumuuisha miradi ya uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini katika mipango ya maendeleo na mikakati ya kitaifa;
7. Kuwezesha na kuratibu upatikanaji wa taarifa za utafiti katika wa sekta ya uvuvi;
8. Kukusanya na kuchapisha takwimu za kitaifa kwenye maendeleo ya sekta ya uvuvi kwa mujibu wa viashiria vya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050;
9. Kutoa muongozo kwa Wizara, Idara na Asasi za Serikali katika utekelezaji wa ajenda, shabaha na mikakati ya kitaifa; na
10. Kuratibu utekelezaji wa miradi ya sekta ya uvuvi iliyoelekezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026.

### 5.3.3 5.3.3 WIZARA ZENYE DHAMANA YA USIMAMIZI KULINDA NA KUHIFADHI MAZINGIRA NA USIMAMIZI WA MAAFA

1. Kulinda uvuvi mdogo mdogo na uvuvi wa bahari kuu kutokana na Kuwakinga na kuwahifadhi wavuvi kwenye maji ya ndani, ya kitaifa na bahari kuu kuu dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya bahari, kwa kushirikiana na wadau wengine;
2. Kushiriki katika kulinda na kuhifadhi maeneo tengefu;
3. Kuwalinda Kuwakinga samaki wenye tabia ya kuhamahama dhidi ya matumizi ya zana haribifu; na
4. Kushiriki utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na maafa.

### 5.3.4 5.3.4 WIZARA ZENYE DHAMANA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

1. Kuoanisha sera za biashara, viwanda na uvuvi ili kuwezesha mazingira ya uwekezaji;
2. Kuimarisha masoko ya bidhaa za uvuvi na kurasimisha biashara zinazohusiana na shughuli za uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini; na
3. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wawekazaji na wafanyabiashara kiufundi ili kuziunga mkono asasi za wawekezaji na biashara katika sekta ya uvuvi.

### 5.3.5 WIZARA YENYE DHAMANA YA UTALII NA MICHEZO

1. Kutekeleza utalii endelevu unaozingatia ulinzi na uhifadhi wa mifumo ya ikolojia ya baharini, maeneo ya fukwe, mafungu, na maeneo mengineyo ya mazingira ya pwani;
2. Kuimarisha uhusiano miongoni mwa Wizara, Idara, Mashirika na wadau wa utalii;
3. Kushughulikia ulinzi na usalama wa masuala ya utalii;
4. Kutumia fursa za utalii endelevu kuongeza ajira zenye staha na upatikanaji wa fedha za kigeni;
5. Kuratibu na kuweka mazingira bora ya uvuvi wa kitalii wa mawindo.Kuweka utengemano bora katika michezo na burudani za baharini; na
6. Kuweka na Kuimarisha Kukuza mazingira rafiki katika michezo na burudani yza baharini.

### 5.3.6 WIZARA YENYE DHAMANA YA SERIKALI ZA MITAA, ASASI ZA KIRAIA NA VIKOSI MAALUM

1. Kuimarisha miundombinu ya masoko ili kuinua biashara na ujasiriamali kwa wanajamii;
2. Kusimamia sera za mazingira na kwa kuimarisha mifumo ya motisha (kama vile kutambua rasmi jitihada za wawekezaji na wana jamii) na uwajibikishaji (adhabu stahiki kwa wenye hatia).
3. Kuwezesha jamii kushiriki katika ulinzi na uhifadhi wa ukanda wa pwani;
4. Kujenga uwezo wa taasisi, hasa Kikosi Maalaum cha Kuzuia Magendo (KMKM), katika kusimamia utulivu na usalama wa baharini, pamoja na uokozi;
5. Kuratibu ushirikiano na mamlaka za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania katika kuimarisha utulivyu na usalama wa baharini;
6. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Wizara, Idara na Mashirika mbalimbali ya Serikali; na
7. Kushajihisha jamii katika kuchangia, kumiliki na kusimamia miradi yao ya kijamii.

### 5.3.7 WIZARA YENYE DHAMANA YA NISHATI

1. Kuimarisha vyanzo vya uhakika vya upatikanaji wa nishati ya umeme wa kutosha ili kujihami dhidi ya uwezekano wa kukosekana kwa umeme kutoka Tanzania Bara;
2. Kukuza vyanzo vya asili vya uzalishaji wa nishati hapa Zanzibar; na
3. Kuhamasisha uunganishaji katika gridi ya taifa kwa vyanzo vya nishati mbadala ya baharini.

### 5.3.8 WIZARA ZENYE DHAMANA YA JINSIA, VIJANA NA UWEZESHAJI

1. Kuwawezesha wanawake katika miradi ya sekta ya uvuvi;
2. Kuweka mazingira rafiki ili kuwasaidia wanawake katika biashara zao katika sekta ya uvuvi;
3. Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika kusimamia miradi na programu zao za maendeleo;
4. Kuwezesha na kujenga uwezo wa vijana kwa maendeleo yao;
5. Kuimarisha utekelezaji wa miradi ya sekta ya uvuvi;
6. Kuimarisha ushiriki wa vijana katika kusimamia miradi na programu za maendeleo yao;
7. Kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ili kuwasaidia vijana katika maendeleo yao; na
8. Kuiwezesha jamii kupata mikopo na ruzuku yenye masharti nafuu itakayowawezesha kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini.

### 5.3.9 WIZARA YENYE DHAMANA YA USAFIRISHAJI BAHARINI NA MIUNDOMBINU

1. Kuhakikisha kusimamia utekelezaji wa sheria za baharini;
2. Kuzuia uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya baharini unaotokana na Kudhibiti na kuzuia umwagikaji wa mafuta pamoja na kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya baharini kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini ya Zanzibar;
3. Kuimarisha miundombinu ya baharini kwenye maeneo yote ya Zanzibar; na
4. Kuimarisha uwezo wa kiutendaji kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya matumizi ya vifaa na vyombo vya baharini kwa wawekezaji.

### 5.3.10 WIZARA YENYE DHAMANA YA AFYA

1. Kudhibiti maradhi ya miripuko na magonjwa mengine ya kuambukiza miongoni mwa jamii za wavuvi; na
2. Kuimarisha kanuni na kudhibiti maadili ya usafi wa mazingira kwenye miundombinu, vifaa vya kusarifu kusindika samaki, na bidhaa za mazao ya baharini uvuvi.

### 5.3.11 WIZARA ZENYE DHAMANA YA MALIASILI NA ARDHI

1. Kulinda na kuhifadhi maeneo ya mikoko na wanyama pori dhidi ya athari zinazosababishwa na shughuli za mbaya za shinikizo la binadamu kwenye matumizi ya maliasili za baharini na mwambao;
2. Kuratibu mfumo jumuishi wa usimamizi wa miundombinu ya sekta ya uvuvi kwenye maeneo ya baharini na pwani, pamoja na kushiriki kwenye mchakato wa Upangaji wa Matumizi wa Maeneo ya Bahari; na
3. Kurasimisha madago na madiko ya uvuvi.

### 5.3.12 WIZARA YENYE DHAMANA YA UWEKEZAJI

Kuimarisha uwekezaji endelevu na ushirikiano kwenye ubia baina ya sekta binafsi na za umma katika miradi ya sekta ya uvuvi.

### 5.3.13 WIZARA YENYE DHAMANA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kuunganisha ujuzi na maarifa ya fani za uvuvi, ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini katika mitaala ya vyuo vya amali na skuli za sekondari.

### 5.3.14 WIZARA ZENYE DHAMANA YA HABARI NA TEKNOLOJIA

1. Kuhamasisha na kuongeza uwelewa wa miradi ya uvuvi kwa wadau kuwekeza katika miradi ya sekta ya uvuvi;
2. Kujenga uwezo wa vyombo vya habari kutoa kwa wakati taarifa za maendeleo ya uvuvi; na
3. Kushajihisha matumizi ya teknolojia katika ya uchumi wa bahari.

### 5.3.15 TAASISI ZENYE DHAMANA YA UTAFITI KWA MAENDELEO

1. Kufanya utafiti kwa mambo yanayohusiana na wa shughuli za uvuvi;
2. Kupeana taarifa za kisayansi na Wizara yenye dhamana ya uvuvi;
3. Kufanya utafiti jumuishi baina ya Wizara yenye dhamana ya uvuvi na taasisi za utafiti za kikanda na kimataifa;
4. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uvunaji endelevu wa rasilimali za baharini;
5. Kuanzisha kituo cha utafiti na kanzidata ya hifadhi ya bahari (CMORDBS), pamoja na mfumo wa upashanaji habari wa ikolojia ya bahari; na
6. Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kufanyia tafiti za kisasa za uvuvi Kuimarisha kanzi data kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa takwimu na upatikanaji wa taarifa kwa wakati.

### 5.3.16 AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

1. Kuimarisha uhusiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa; na
2. Kushirikiana na Ofisi ya Mambo ya Nje katika kuratibu masuala ya Zanzibar.

### 5.3.17 SEKTA BINAFSI NA ASASI ZA KIRAIA

1. Kushiriki katika utekelezaji wa sera pamoja na programu za sekta ya uvuvi;
2. Kuipa mazingatio maalum na kuiingiza miradi ya maendeleo ya uvuvi katika programu na mipango ya kitaifa;
3. Kushajihisha utoaji wa kipaumbele katika kuiendeleza sekta ya uvuvi;
4. Kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine katika kukuza fursa za uwekezaji, ajira zenye staha, na kupunguza umasikini; na
5. Kuwezesha Kushiriki katika uwekezaji katika maeneo ya usarifu, huduma za masoko, ongezeko la thamani, na kuinua uwezo wa kuwekeza miongoni mwa wafanyabiashara na wajasiriamali.

### 5.3.18 WASHIRIKA WA MAENDELEO

1. Kusaidia katika kuunganisha mipango ya maendeleo, pamoja na upangaji wa programu na upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuwezesha kufikiwa kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi kitaifa.
2. Kushiriki katika kuimarisha ujuzi na uwezo wa kiufundi wa wataalamu ili kwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia na uzoefu wa kimataifa katika maendeleo ya sekta ya uvuvi.



# SURA YA SITA
# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 6.1 MFUMO WA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa Sera ya Uvuvi umetayarishwa ambao unaenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, utakuwa na vipengele muhimu vifuatavyo: mpango wa utekelezaji, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, mapitio ya sera, rasiliamali fedha na bajeti, pamoja na mkakati wa mawasiliano. Mipango na bajeti itaratibiwa na taasisi husika kwa kutumia Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) na mipango mkakati ya kisekta.

## 6.2 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na tathmini ni muhimu katika kutekeleza sera hii na kupima matokeo ya utekelezaji. Jukumu la jumla la ufuatiliaji na tathmini ya Sera hii ipo chini ya Wizara yenye dhamana ya shughuli za uvuvi,ufugaji na kilimo cha mazao ya baharini. Aidha mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji kwa kutumia viashiria muhimu vya maendeleo endelevu kwenye ngazi ya kitaifa na kimataifa.

## 6.3 MAPITIO YA SERA

Wizara yenye dhamana ya uvuvi itafanya mapitio ya sera, kufuatana na miongozo, kila baada ya miaka mitano (5) au itakapohitajika kufanywa hivyo. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na maoni ya wadau yatatumika katika kuelewa maendeleo ya kijamii, kisiasa, kimazingira na kiuchumi; na pia kuarifu iwapo ipo haja ya kufanya mapitio.

## 6.4 GHARAMA NA RASILIMALI FEDHA

Wizara yenye dhamana ya fedha itakuwa na wajibu wa upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha , Wizara yenye dhamana ya fedha kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya uvuvi zitaandaa bajeti mahususi ya kukidhi malengo ya utekelezaji.

## 6.5 MKAKATI WA MAWASILIANO

Wizara yenye dhamana ya uvuvi itatayarisha mkakati wa mawasiliano wa utekelezaji wa Sera ya uvuvi, ambao utahusisha upashanaji wa habari na mawasiliano, upatikanaji na usambazaji wa taarifa, machapisho pamoja na utekelezaji wa malengo na shabaha. Mkakati utaoanisha maendeleo yanayofikiwa katika juhudi za utekelezaji miongoni mwa taasisi za serikali na binafsi, na washirika wa maendeleo. Mkakati pia utaitangaza na kuitambulisha sera ya uvuvi katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa; kubainisha vipaumbele vya sekta ya uvuvi kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar; na kutoa wito kwa jamii za kimataifa na washirika wa maendeleo kushiriki katika kuwekeza kwenye maendeleo ya sekta ya uvuvi nchini.

## 6.6 RASILIMALI WATU

Mkakati wa rasilimali watu utatekelezwa sambamba na mpango wa ufuatiliaji na tathmini. Mkakati utabainisha rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji wa sera hii kwa kuzingatia mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi. Aidha, mkakati wa rasilimali watu utachambua mahitaji ya rasilimali fedha, teknolojia, na miundombinu ili kujenga uwezo na kupata ufanisi kwenye maendeleo ya sekta ya uvuvi.





**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR**

Maisara Area, ZURA Building
Ground Floor, Room No.06
P.O.Box 149

+2550242941195

info@blueeconomysmz.go.tz